


KUNG'ANG'ANIA

 Asante, Ndugu Parker.

² Ni majaliwa kuwa hapa. Nasikitika kwamba nilichelewa kidogo, lakini ugonjwa mbaya sana nyuma ya pazia, mnaona, nilikuwa nikimhudumia huyo mtoto mchanga.

³ Basi nina furaha sana kuwa hapa tena, usiku wa leo, nami ninatumaini ya kwamba sitawaweka kama nilivyofanya jana jioni. Niliwaweka muda mrefu sana, na—nami nikaenda nyumbani, na kwa namna fulani nilijisikia, ama, nilienda kwenye moteli yangu na kwa namna fulani nikajisikia vibaya, nilipoona ilikuwa ni saa ngapi, nilikuwa nikizungumza hapa kwa yapata saa moja na dakika arobaini na tano.

⁴ Na bila shaka, huo ni—huo ni muda mfupi kwangu, hivi majuzi nilizungumza kwa saa sita. Mnaona, endapo jamaa fulani anajua mengi sana, haimbidi kuzungumza kwa muda mrefu sana, lakini wakati hujui mengi sana, inakubidi tu kujazia, mnajua, nadhani. Na, mnaona, mimi humngojea tu, ndipo—ndipo ninapojisikia kwamba Yeye amenipa jambo la kusema, vema, basi ni—ninalisema, nami kwa namna fulani inanibidi kuendelea nikiyumbayumba mpaka wakati huo.

⁵ Nilikuwa nikijaribu kuzungumza jana usiku kuhusu kutoa hoja, sio, wakati kitu chochote kinapotoa hoja dhidi ya Neno la Mungu. Simaanishi hoja, *hoja* yoyote tu, kwa sababu Paulo alihojiana na watu. Basi shida siku hizi, watu huchukua tu chochote kinachokuja, wala hawalihoji kwa Maandiko. Lakini wakati ni—ni kutoa hoja *dhidi* ya Neno la Mungu, basi kaa mbali nalo, huyo ni adui. Unaona? Lakini wakati ni kuhojiana *na* Neno la Mungu, huyo ni Mungu, mnaona, hilo ni jema; hoja hizo mbili. Kwa hiyo tunaamini katika kuhojiana na Neno, tunaamini ya kwamba Neno ni sahihi.

⁶ Sasa, huwezi kulithibitisha Neno kisayansi, kwa sababu kama . . . wala kamwe hutalithibitisha, kwa sababu ni kinyume sana na sayansi. Kama likithibitishwa kisayansi, basi si imani tena. Mnaona? Huna budi kuwa na imani, na imani ni kinyume na kuthibitisha kisayansi. Kwa hiyo huna budi kuliadini, si kulithibitisha, kuliadini, wazo ndilo hilo.

⁷ Wakati fulani uliopita nilikuwa nikizungumza na mtu fulani, nilikuwa huko Toronto, Canada, tulikuwa na mkutano mkubwa kule, naye Bwana alikuwa akibariki kwa njia ya ajabu sana. Nilikuwa upande wa pili katika . . . Haikuwa huko Toronto, sasa, ninalighairi hilo, ninasahau majina ya mahali hapo huko Canada tulipokuwa tukiufanyia huo mkutano. Nitalikumbuka katika dakika chache. Nimesafiri sana hata siwezi kukumbuka majina ya mahali hapo wakati mwingine. Na pako moja kwa

moja upande wa pili kutoka Detroit. [Mtu fulani anasema, “Windsor?”—Mh.] Ati ni jina gani? [“Windsor.”] Windsor, sawa; Windsor, Ontario.

⁸ Basi kulikuwako na...kulikuwako na televisheni moja imewekwa mtaani, namna fulani ya skrini, na kulikuwako na kaoboi kule akicheza, akipiga gita, huko, akitangaza kutoka Marekani. Ndipo huyo mtu akatokea, naye alikuwa akizungumza nami. Kasema, “Ningetaka kukuuzia hiyo.”

Kasema, “La, Bwana, tulikuwa tunapita tu.” Nikasema, “Siamini ninaitaka.”

Naye akasema, “Vema, nitakuuzia rahisi kweli.”

Nami nikawazia...Nikamwelezea, nikasema, “Mimi ni m—mtalii.” Nikasema, “Mimi...”

“Loo,” kasema, “unapita tu, nadhani?”

Nikasema, “La, niko hapa chini kwenye moteli.” Nikasema, “Niko hapa kwa siku chache tu.”

Kasema, “Huko kwenye mkutano ule kule?”

Nikasema, “Naam, Bwana. Hiyo ni kweli.”

Akasema, “Sitaki kuudhi hisia zako, lakini,” kasema, “mnamsikiliza tapeli.”

Ndipo nikasema, “Woo!” Nikasema, “Hiyo ni...Naam, Bwana,” nikasema, “unafikiri hivyo?”

Akasema, “Naam, Bwana,” akasema, “Naam.”

Nami nikasema, “Vema, kwa nini utoe maamu...maoni ya hilo?”

Akasema, “Vema, kwa sababu mtu huyo anazungumza juu ya kitu ambacho hajui lolote kukihusu.”

Nami nikasema, “Unamaanisha nini?”

⁹ “Vema,” akasema, “kwa mfano, jana usiku, yule askari pale, aliyekuwa jeshini, naye amelala kwenye machela hii, naye alikuwa...akidhaniwa amepooza.” akasema, “Niliamka na kuzunguka pale,” kasema, “hilo lilikuwa ninii, huyo alikuwa akijifanya,” kasema, “mtu huyo alimjua mtu huyo wakati wote.” Kasema, “Alikuwa tu amelala pale akijifanya.”

¹⁰ Nikasema, “Kwa nini hukumwendea huyo mtu aliyekuwa kwenye machela na kuchunguza, uone alikuwa ni nani, mahali alikotoka? Kama ungalikuwa na shauku kubwa sana, hivi hudhani ulipaswa kufanya hivyo?”

Akasema, “Vema, hili hapa jambo lote,” akasema, “Sijaribu kukuvunja moyo.”

Nikasema, “Loo, hutaweza.”

Kwa hiyo akasema—akasema, “Na—nafikiri kwamba... Ninaamini katika sayansi.”

Nikasema, “Nami pia.”

Akasema, “Vema, chochote ambacho hakiwezi kuthibitishwa kisayansi si sahihi.”

Nikasema, “Simaanishi kuwa tofauti, bali ninasema tu hilo ni vinginevyo. Chochote. . .”

Akasema, “. . . si halisi.”

¹¹ Nami nikasema, “Chochote kinachoweza kuthibitishwa kisayansi si halisi.” Nikasema, “Mambo ambayo hayawezi kuthibitishwa kisayansi ndiyo yanadumu na ni halisi.”

¹² “Loo,” akasema, “hilo si kweli.” Mnaona? Na—na sasa, akasema, “Angalia hapa yale sayansi imefanya.” Kwanza alisema hivi, akasema, “Vema,” akasema, “Siamini.”

Nikasema, “Vema, ninataka kukuuliza jambo fulani. Wewe ni mtu ambaye ameo?”

Akasema, “Naam.”

Nikasema, “Unampenda mkeo?”

Akasema, “Bi—bila shaka ninampenda.”

Nikasema, “Nami pia. Ninathamini hilo. Lakini. . .”

¹³ Je, ninafanya. . .? [Mtu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Loo. Vema sasa? Samahani, si—siwezi kujua hilo hapa, mnaona.

¹⁴ Kwa hiyo—kwa hiyo wakasema—kasema, “Kama wewe. . . Chochote usichoweza kuthibitisha kisayansi ni—ni uongo.”

Nikasema, “Vema, sasa, unampenda mke wako tofauti na mwanamke mwingine yeyote?”

“Naam.”

Nikasema, “Ni kitu gani hicho?” Mnaona? Mnaona? “Una watoto? Ni kitu gani kinachowafanya hao watoto kuwa tofauti na watoto wengine wowote?”

¹⁵ Akaendelea kuzungumza kwa dakika chache tu, naye akasema, “Vema,” akasema, “sasa, kwa mfano *hii*,” akasema, “unaona, hakuna waya kuizunguka mahali popote.”

¹⁶ Nikasema, “Hiyo ni kweli, na hilo ni jambo kuu.” Nikasema, “Sasa, hili hapa, mtu huyo yuko Marekani, na bila waya wala chochote kilichounganishwa nayo, Marekani, kupitia kwa mawimbi, namna fulani ya mawimbi ya elektroniki ya chochote kile, yanaleta picha ya mtu huyo hapa kikamilifu tu, na kuiakisi pale.”

Akasema. . . Ndiyo kwanza aseme asingeweza kuelewa jinsi upambanuzi huo, kasema, “Nafikiri ni shughuli tu iliyopangwa.”

¹⁷ Nikasema, “Loo?” Kwa hiyo nikasema, “Sasa, *hiyo* si shughuli ya kujitengenezea, usingesema hivyo,” Nikasema, “kwa sababu kweli kabisa, kuna wimbi linalopitia hapa, ambalo. . .”

nasi tumefundishwa ya kwamba picha iyo hiyo inakuja moja kwa moja kupitia kwetu. Na kwamba ujumbe, na kwamba nyimbo, na kila kitu kinapitia moja kwa moja kwetu, lakini basi inagonga kioo *fulani*, ama kitu fulani mle ndani, ambacho ni . . . ama tyubu, inayoweza kuakisi picha hiyo, na picha ya huyo mtu, inayosafiri kupitia mawimbi ya etha ya hewani. Wala hatujui inakotoka, inaninii tu . . . tunajua inakotoka, lakini,” nikasema, “hatuwezi kuiona, nayo inapita, na kuiakisi pale.”

¹⁸ Nikasema, “Hivyo ndivyo Mungu . . .” Unaona? Nikasema, “Hivyo ndivyo jamaa huyo anavyojua mambo hayo.” Nikasema, “Unaona, Mungu,” mnaona, “hushusha hilo wimbi la etha chini.” Kisha nikasema, “Huenda likapitia katika maelfu na mamilioni ya watu mpaka itakapofika mahali hapo, ndipo inaiakisi. Hivyo ndivyo yeye . . .”

Akasema, “Loo,” akasema, “hiyo ni sawa, lakini,” kasema, “angalia, unaona, tuna kituo cha kutuma, tuna kituo cha kutuma ambacho hutuma hayo.”

¹⁹ Nikasema, “Na sisi pia.” Tuna Kituo cha kutuma, hiyo ni kweli, Kituo cha kutuma, na kituo cha kupokelea. Kwa hiyo Yeye—Yeye angali ni Baba yetu wa Mbinguni, sivyo? Tunampenda kwa sababu alitupenda kwanza, akamtuma Yesu Kristo apate kufa badala yetu, kusudi Yeye . . . tupate kuwa haki ya Mungu kwa njia ya Kristo, nina furaha sana.

²⁰ Maono hayo wakati mwingine ni . . . kwa namna fulani yanawakwaza watu, hawaelewi. Wakati mwingine watu wanafikiri yanaendelea tu papa hapa mkutanoni. Loo, jamani, hii ndiyo sehemu yake iliyo ndogo. *Huko* nje ndiko yanakotukia kweli.

²¹ Leo hii nilikuwa nimeketi chumbani. Tulikuwa na . . . Kwa kawaida Ijumaa ni siku yangu ya kufunga, mimi sili, wakati mwingine, Jumanne na Ijumaa, mpaka wakati fulani alasiri, kufupi tu . . . huko si kufunga kwa kawaida, huko ni kufunga tu siku chache kwa juma. Kwa hiyo, kufunga kwa muda mrefu huja katika siku nyingi zaidi, wakati Bwana anapoliweka juu yako. Lakini hiyo ni staha na heshima tu ya kumbukumbu kuu ya Mungu kwetu, kule kufunga, amri.

²² Na kwa hiyo, baada ya saa tisa, kwa kawaida hula chakula chepesi. Mtu fulani aliniambia ambapo ungeweza kununua steki ndogo hapa chini barabarani kwa yapata senti tisini, karibu tu sawa, kwako kula. Katika kuhubiri na mambo haya inakubidi kuendelea bila kula. Kwa hiyo tulikuwa tukipanga kwenda kule chini, ndi—ndipo mwanangu na mpwangu wakashangaa ni kwa nini hatukushuka kwenda kule, lakini tukageuka na kwenda kwenye mkahawa mwingine.

²³ Halafu basi, tukiwa tumeketi mle ndani, nikaona . . . Katika dakika chache tulipokuwa tukizungumza, na watu fulani walikuwa pale, kulikuwa na . . . Daima ni vizuri kukutana na

marafiki zangu, mwajua, na kuzungumza nao, na kwa hiyo nilikuwa nimepeana mikono na baadhi ya watu hao.

²⁴ Katika dakika chache, wanawake wawili wakaingia, Roho Mtakatifu akasema, “Yule aliyevaa kofia nyeupe.” Nikazunguka, sijawahi kuwaona maishani mwangu. Na ajabu, wakati mwanamke mmoja alipokuwa akitaka kuketi namna *hii*, akageuka naye alikuwa akinitazama moja kwa moja. Hiyo ni neema, unaona, kujua tu. . . Hakuna kitu kinachotukia kwa bahati. Kwa hiyo alikuwa akiniangalia moja kwa moja.

²⁵ Ajabu, mwanangu mwenyewe, ambaye amesimama pamoja nami hapa jukwaani kwa miaka mingi, lakini akaniuliza swali, jambo fulani kuhusu ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu ama kitu fulani, basi, “Loo,” nikasema, “Billy, sielewi mambo hayo.” Nikasema, “Nina mawazo yangu tu kuyahusu.” Nikasema, “Siyafundishi, kwa sababu hu—huenda nikakosea maili milioni moja kuyahusu. Unaona?” Nikasema, “Nina mawazo yangu tu.”

²⁶ Naye akasema, “Vema, ningetaka kujua kuhusu *hili*,” na *jambo lingne*, ndipo basi, kwa ghafla, hakulipata. . . Wala hajui ninalisema, kuhusu mimi kusema hili sasa, kama yupo. Lakini iwapo Charlie na Billy wako karibu, hivi uliona, Charlie? Mara Billy akabadilisha ikawa neema upesi sana, kuhusu neema ya Mungu kudumisha.

²⁷ Mnaona, yeye hakutambua dakika hiyo, Bwana alikuwa amenipa mawasiliano na roho ya mwanamke huyo. Naye huyo hapo. Hakuwa na hakika sana ilikuwa ni mimi, maana alikuwa tu ameniona jana jioni. Nikawazia, “Bwana, ninamwona huyu mwanamke, hali aliyo nayo, na kile kilichotukia.” Nikawaza, “Labda yuko kwenye mkutano.” Nilijua alihitaji msaada.

²⁸ Na mara tu, wakati, baada ya kumaliza chakula chetu cha kutwa, wengine, kabla ya kumaliza, maskini dada fulani mzuri kutoka huko chini mahali fulani alikuja, akalipia chakula changu cha kutwa, kwa hiyo basi. . . yeye na mumewe, na watoto.

²⁹ Na kwa hiyo, ndipo nikaamka kwenda kulipia hicho chakula cha kutwa. Nami nadhani Billy na Charlie waliona niliwaacha waendeleo, kwa sababu nilijua mama huyo alikuwa anakuja mahali fulani, maana nilijua alikuwa nyuma yangu, katika dakika chache akanena nami. Na hapo niliweza kumwambia huyo mama yale hasa yaliyokuwa yametokea, yale yaliyotukia, na si kwa bahati, bali huo ulikuwa ndio mwanzo wa uponyaji wake.

³⁰ Miaka mingi iliyopita, yeye nadhani alikuwa mwanamke wa karibu miaka sitini ama kitu kama hicho, na katika wakati wa kukoma hedhi alikuwa ameshikwa na wasiwasi sana, wala hakuweza kujiondoa kwake. Na ninii. . . Akasema, “Nilikusikia mara moja tu, ninatoka mbali sana, hiyo ilikuwa jana usiku.” Akasema, “Tamshi lile ulilotoa kuhusu kuvunja

kizuizi hicho cha sauti, upate kuwa huru,” akasema, “siku nzima nimehangaika na kizuizi hicho cha sauti.”

³¹ Nikasema, “Usihangaika tena.” Mnaona? “Imekwisha sasa. Unaona? Um-hum. Kivuke.” Nami nikasema, “Kizuizi cha sauti ni kizuizi kati ya imani na kutokuamini. Unapopita kutokuamini huko kwa kivuli cha shaka, uko huru basi, unaona, hakuna ki- . . .”

³² Naye huyo mama alikuwa, katika wakati huo alikuwa ameninii. . . Jinsi wakati mwingine kukoma hedhi, hasa ama kuingia, au kukoma, huwafanya watu kuwa na wasiwasi sana. Wala kamwe hakuwa ameweza kupitia hayo. Huyo mwanamke huwazia wakati mwingine ya kwamba amepotea, ndipo anangia wazimu. Naye, ni mwaminio Mpentekoste, nafikiri ndivyo, lakini huyo mama alikuwa amevaa. . . amejipodaa, na nywele fupi, na kila kitu, lakini sababu ya yeye kufanya hivyo, alikuwa akijaribu kuachna na hayo, mnaona, akijaribu kujiondoa kwenye hisia hizo za kutisha.

³³ Nasi tulianza tu kuzungumza juu ya. . . Mnaona, hivyo ndivyo. . . Billy hajui sasa kwamba ninasema hili, wala Charlie. Hivyo ndivyo neema. . . sababu ya wewe kujisikia hivyo, Billy, ukiongea kama kinanda, mwajua, “Neema, i—inakuwaje ni—ni *hivi*? Na inakuwaje *hivyo*? Na vipi, unajua, *fulani-na-fulani*?”

³⁴ Nikasema, “Ni neema ya Mungu. ‘Wale aliotangulia kuwajua aliwaita; wale aliowaita, aliwahesabia haki; wale aliowahesabia haki, amewatukuza tayari.’ Yote ni Mungu.” Na hivyo ndivyo ilivyokuwa, wala haimbidi kuwa na wasiwasi juu ya jambo hilo.

³⁵ Alikuwa akijaribu kujiondoa kwenye kitu hicho. Angetoka nje, naye angefanya *hivi* na kufanya *vile*, akijaribu kujiondoa kwake. Lakini leo hii maskini mwanamke huyo aliugonga huo ufunguo, amepona sasa. Naye huenda akawa hapa usiku wa leo, Sijui, ah, huenda alienda nyumbani, lakini huenda akawa hapa, bado usiku wa leo, mkutanoni.

³⁶ Lakini inaonyesha tu jinsi neema ya Mungu itakavyofanya mambo. Iko kwa—kwa wingi sana kuliko yote ambayo tungeweza kufanya wala kuwazia, sivyo? Ajabu.

³⁷ Sasa, kesho asubuhi ni kiamshakinywa, nami nilimwuliza Ndugu Parker kama ilikuwa nizungumze kwenye kiamshakinywa hicho, huku, nikijaribu kukwepa, lakini akasema, la, kwamba nilikusudiwa kusema maneno machache. Halafu basi, kesho usiku, ninataka kujaribu, Bwana akipenda, kuhubiri, kuleta ujumbe mdogo.

³⁸ Nami sidhani nitajaribu tena, kama jana usiku, kwa sababu nilijisikia vibaya sana, huku nimeketi hapa mbele ya waalimu, na waalimu mashuhuri wanaojua, wanatheolojia kama Dk. Lee Vayle, na hawa ndugu wengine wote hapa ninaowajua, jamani, waliohitimu, na kadhalika, ambao—ambao walisoma Biblia, na kufundishwa hiyo, kisha mimi nisimame hapa, nikijaribu kuleta

ujumbe wa aina hiyo. Nilifikiri ningekuja kuwaombea watoto wagonjwa wa Ndugu Parker, kwa hiyo a—afadhali nishike mstari huo. Kwa hiyo tuko hapa kusaidia.

³⁹ Sasa, usiku wa leo, na—nataka kujaribu kuzungumza na kusoma Maandiko fulani, ili kwamba isinichukue muda mrefu sana, kama dakika thelathini ama kitu kama hicho. Ndipo ninataka kuwaombea ninyi wagonjwa usiku wa leo, aminini tu. Sasa, mtu yeyote anajua ya kwamba wanadamu hawawezi kufanya mambo haya, haiwezekani, mnaona, haina budi kuwa ni Roho wa Mungu.

⁴⁰ Na kwa hiyo sisi...Jambo tu tunaloweza kufanya ni kuwaombea wagonjwa. Siwezi kumponya mtu yeyote, kwa sababu tayari mmeponywa. Kama mtu yeyote akikwambia kwamba wanaweza kukuponya, hilo ni kosa. Unaona? Na mtu yeyote anayekwambia wanaweza kukuokoa, hilo ni kosa, umeokoka kwa vyovyote vile. Unaona? Jambo pekee unalopaswa kufanya ni kulikubali tu. Unakubali yale Yesu aliyokufanyia, “Alijeruhiwa kwa makosa yako; kwa kupigwa Kwake uliponywa.” Uliponywa, tayari ni wakati uliopita.

⁴¹ Jambo pekee unalopaswa kufanya ni kukubali yale aliyokufanyia, hivyo tu. Nanyi mko chini ya Damu, kila mmoja wenu, la sivyo Mungu angeangamiza kitu hicho chote. Mngali mko chini ya Damu maadamu kuna Dhabihu iliyojaa Damu iliyowekwa pale kwa ajili ya dhambi zetu. Ndipo siku moja unapoondoka ulimwenguni humu bila kuikubali hiyo Dhabihu, basi unasimama kwa ajili ya dhambi zako mwenyewe, nawe tayari umehukumiwa, unaona, kwa hiyo huwezi kusimama.

⁴² Na uponyaji wako ni ninii tu...Mungu alifanya njia nzuri sana. Unaona, imani huja kwa kusikia. Hubiri uponyaji wa Kiungu, uamini, ukubali. Hiyo...Kama huyo angekuwa ni mimi, hivyo ndivyo ningelifanya, usingeweza kuamini neno langu, vema, nawe ungekuwa vivyo hivyo kwa mtu mwingine yeyote, bali si Mungu. Baada ya Yeye kutuma Neno Lake, ndipo Yeye huweka Kanisani karama mbalimbali na kadhalika, ili, kujaribu tu kuwaletea watu ninii...Yeye ni mwenye upendo sana na mwingi wa fadhili.

⁴³ Hebu na tufungue sasa, katika Kitabu cha Mathayo Mtakatifu, Injili ya Mathayo Mtakatifu mlango wa 15, kifungu cha 21 hadi cha 28. Mathayo Mtakatifu, mlango wa 15, kifungu cha 21 hadi cha 28. Sikilizeni kwa makini, kusomwa kwa Neno.

Yesu akaondoka huko, akaenda kando pande za Tiro na Sidoni.

Na tazama, mwanamke Mkananayo wa mipaka ile akatokea, akampazia sauti akisema, Unirehemu, Ee Bwana, Mwana wa Daudi; binti yangu amepagawa sana na pepo.

Wala yeye hakumjibu neno. Nao wanafunzi wake wakamwendea, wakamsihi wakisema, Mwache aende zake; kwa maana anapiga kelele nyuma yetu.

Akajibu, akasema, Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli.

Naye akaja akamsujudia, akisema, Bwana, nisaidie.

Akajibu, akasema, Si vema kukitwaa chakula cha watoto na kuwatupia mbwa.

Naye akasema, Kweli, Bwana: lakini hata mbwa hula. . . makombo yaangukayo kutoka mezani pa bwana zao.

Ndipo Yesu akajibu, akamwambia, Mama, imani yako ni kubwa: na iwe kwako kama utakavyo. Akapona binti yake tangu saa ile.

⁴⁴ Hebu na tuinamishe tu vichwa vyetu sasa, tunapozungumza na Mwandishi wa Neno hili.

⁴⁵ Baba wa Mbinguni mwenye rehema, sasa tunakaribia madhabahu Yako matakatifu katika Jina la Bwana Yesu. Na yote yanatosha, yote tunayohitaji, kwa sababu Yeye alisema, “Mkimwomba Baba lolote katika Jina Langu, nitalifanya.” Kwa hiyo, tusingeweza kuja kwa jina letu wenyewe, ama jina la kanisa, ama kusanayiko lolote, wala taifa lolote au jamii, tunakuja tu kwa urahisi katika Jina la Bwana Yesu, nasi tunajua ya kwamba utatusikia, kwa sababu Yeye alisema ungetusikia.

⁴⁶ Wala hatuombi, usiku wa leo, kusimama kwenye Kiti cha Enzi cha Hukumu Yako, kwa kuwa tungehukumiwa, lakini tunaomba kusimama kwenye Kiti cha Enzi cha rehema, ambacho sote tunakikimbilia.

⁴⁷ Sasa, Bwana, ninatambua uzito mkubwa mno wa huu mkutano, na jinsi ambavyo hapana shaka zilimwagwa kutoka Kwako, nguvu hizi, ulipoangalia umati wa wagonjwa, viwete, vilema, vipofu, uliposimama kwenye birika la Bethesda na kuona umati huo mkubwa, hata hivyo, kulikuwa na mtu mmoja tu uliyeongozwa wake, Nawe ulisema ulijua alikuwa hivyo kwa muda mrefu, Nawe ukamponya, au, ukamwomba aukubali.

⁴⁸ Ndiposa, ulipoulizwa, Wewe ulisema, “Amin, nawaambieni, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba analitenda.” Bwana, hivi hutatuonyesha mapenzi ya Mungu, usiku wa leo, kwa ajili ya umati huu mgonjwa, unaongojea? Tunangojea kutibuliwa kwa maji, kusudi wagonjwa wapate kuingia na kuponywa.

⁴⁹ Ninakuomba, Mungu, utusamehe dhambi yetu ya kutokuamini, maadamu tumekuwa tukikufuata Wewe. Nasi tunakiri, Bwana, ya kwamba tumepungukiwa kabisa na masharti kama wahudumu na kama Wakristo, kwa hiyo uturehemu, Ee Mungu wa Rehema.

50 Na kama vile mtu mmoja alivyolia siku moja, akiwa pamoja na mvulana mwenye kifafa, kasema, “Bwana, saidia kutokuamini kwangu,” tunakulilia Wewe, usiku wa leo, Bwana. Baada ya kusoma ahadi za Biblia hii ya thamani na kuona yale yangeweza kufanywa, ndipo tunalia, “Saidia kutokuamini kwetu.” Tuma Uwepo wa Bwana Yesu miongoni mwetu, usiku wa leo, tunapozungumza juu ya Neno. Basi jalia Neno lifanyike mwili, na roho zetu zilishike, tuliamini.

51 Jalia tuone kurudi kunakokaribia kwa Bwana Yesu, kama alivyoahidi, wakati siku zikizidi kusonga mbele sasa katika dakika na saa, ama labda saa na dakika. Nasi hatujui tuko karibu vipi, Bwana, bali tunaona mambo yanakuwa, yakionekana kuiva, kwa hiyo tusaidie, usiku wa leo.

52 Tunaliwasilisha Neno Kwako, usiku wa leo, Baba, kwamba utalibariki. Pata heshima kwa Jina Lako, Jina ambalo kwalo tunaomba, la Bwana Yesu, na kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

53 Ningejaribu kutoa kutoka kwenye fungu hili dogo, usiku wa leo, ama, Andiko hili, kwa dakika chache tu juu ya somo, ama neno linaloitwa *Kung'ang'ania*. Ninatoa hilo kutoka kwenye vifungu ambavyo nimesoma hivi punde. *Kung'ang'ania*, ni “kuweka lengo, kushikilia.” Ninapenda hili neno, nalo, linafaa sana kwa Kanisa la siku hizi, ama inapaswa kuwa kwamba Kanisa linapaswa kung'ang'ania.

54 Watu wa nyakati zote walio na imani katika yale wanayojaribu kufanikisha wamekuwa waking'ang'ania. Haidhuru unajaribu kufanya nini, huna budi kuamini katika yale ufanyayo.

55 Mtu mmoja wakati mmoja aliniambia, daktari, alisema, “Loo, ninaamini, Ndugu Branham, kama—kama watu wangeamini ya kwamba wangeweza kwenda na kuugusa mti ule nao wangeponywa, ninaamini ingetendeka.”

56 Nikasema, “Lakini ndugu yangu wa thamani, watu hawawezi kuwa na imani katika kuugusa mti ule. Imani haina budi kuwekewa msingi juu ya jambo fulani, na kwa hiyo, wakati mtu anapoweza kuwekea msingi imani yake juu ya Neno la Mungu, basi unaweza kushikilia kwa sababu ni Neno la Mungu.”

57 Kama vile maskini yule ndugu alivyosema, ndugu mweusi, huko chini katika majimbo ya kusini, alisema afadhali awe akisimama juu ya Neno kuliko Mbinguni, ndipo mtu fulani akamwuliza ni kwa nini, akasema, “Kwa sababu ‘Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita.’” Basi hiyo ni kweli.

58 Ukisimama juu ya Neno, ndipo unaweza kupata jambo fulani, si yale mtu mwingine aliyosema, yale shule fulani iliyofundisha, yale mhudumu fulani aliyosema, yale daktari fulani aliyosema, bali ni BWANA ASEMA HIVI, ndipo unaweza kushikilia.

59 Na mtu yeyote anayefanya jambo lolote, kama wanajaribu kufanikisha jambo fulani, lazima kwanza wawe na imani ya kuamini jambo hilo, kama vile baba wa taifa letu, anavyoitwa, rais wetu wa kwanza, George Washington. Juu kidogo tu huko pwani, nilipokuwa nikisoma hapa miaka michache iliyopita kuhusu Washington, nilikuwa nimewaona, ambapo walikuwa na koti lile ambalo risasi zilipitia.

60 Nasi tunaambiwa ya kwamba usiku uliotangulia Valley Forge, wakati alipovuka huo mto, akiomba usiku kucha, mpaka ninii yake, moja kwa moja juu ya nyonga zake alikuwa amelowa mahali alipopiga magoti kwenye theluji, alikuwa akitafuta mapenzi ya Mungu maana upinzani ulionekana kuwa mkubwa. Delaware ulikuwa umejaa barafu, karibu nusu ya askari wa Marekani walikuwa na viatu miguuni mwao, ilionekana kana kwamba alikuwa amelemazwa, bali alimkimbilia Mungu.

61 Ndipo kesho yake akavuka Bonde la Forge. Aling'ang'ania. Risasi zilipitia kwenye koti lake na kamwe hazikumgusa. Alikuwa akijaribu kufanikisha jambo fulani, kwa hiyo akamtafuta Mungu na kupata jibu, ndipo angeweza kung'ang'ania.

62 Hivyo ndivyo tunavyofanya. Inakubidi kwanza kutafuta mapenzi ya Mungu kabla hujaweza kufanya mapenzi ya Mungu. Lazima kwanza ujue mapenzi Yake ni nini katika jambo hilo, ndipo basi usiyaachilie. Na kama vile yule mama alivyosema leo, alikuwa akijaribu kuvuka kizuizi hicho cha sauti, basi hiyo ndege inashika tu mwendo na kwenda bila kikomo, inapopita kizuizi cha sauti.

63 Vema, unapoweza kuomba mpaka upite kizuizi cha shaka, basi uko huru, unaweza kuendelea. Halafu unaninii . . . hakuna kitu kinachoweza kukusumbua basi, kwa sababu uko huru, umepita kutokuamini, tayari yametatuliwa, yote yamekwisha. Unapopata hakikisho moyoni mwako ya kwamba itakuwa hivyo, una furaha tu kana kwamba tayari imetendeka.

64 Kwa mfano, labda mkate mmoja, kama nilikuwa na njaa na mkate mmoja ungeyaokoa maisha yangu, nami ningomba mkate, ndipo mtu fulani angenipa senti ishirini na tano, na hiyo ndiyo bei ya kununua mkate, ninaweza nikawa tu na furaha nikishika hizo senti ishirini na tano mkononi mwangu kadiri ninavyoweza nikishika mkate, kwa sababu ndizo uwezo wa kununua. Amina. Mimi . . . Basi ninao, sina mkate, bali nina uwezo wa kununua, vema, hiyo ni imani.

65 Unapoweza kuomba mpaka upate hakikisho, unaweza kufurahia vivyo hivyo kama kansa imetoweka, upige kelele kwa sauti kuu vivyo hivyo, kwa sababu unao uwezo wa kununua, imani inayokiendesha kitu hicho, basi unang'ang'ania. Hakuna mtu anayeweza kukwambia jambo lolote tofauti, haijalishi mtu

yeyote anasema nini basi, tayari umevuka kizuizi cha sauti, uko huru basi; kununua na kung'ang'ania.

⁶⁶ Nuhu, kama tulivyozungumza juu yake jana usiku, ama, kumhusu, alipoisikia Sauti ya Mungu ikinena naye na kumwambia juu ya hukumu ijayo, baada ya kusikia Sauti ya Mungu ikimpa u—ushahidi wa yale yatakayotukia, na kumjenga, ama, kumwagiza, hasa, samahani, la kufanya, alishikilia sana.

⁶⁷ Wenye kudhihaki hawakuwa na kitu. Haidhuru ni makasisi wangapi waliosimama na kusema, “Nuhu, umekosea,” alishikilia moja kwa moja, akajenga safina hata hivyo. Wenye kudhihaki wangeweza kumkaribia kwa maelfu na kusema, “Mwangalieni maskini yule mzee, mtazameni!”

⁶⁸ Sayansi ingeweza kusimama pale, na kusema, “Nuhu, angalia hapa, jamani, tunakupenda, lakini umerukwa na akili. Tuna chombo hapa kinachoweza kurusha kote kote hadi mwezini, nasi tunaweza kuthibitisha ya kwamba hakuna mvua wala maji kati ya hapa na huko ambayo yangeizamisha dunia. Angalia katika chombo hiki, kitathibitisha jambo hilo.”

⁶⁹ Nuhu angeninii . . . huenda angesema kitu kama hiki: “Sijali kile chombo chenu kinachosema. Mnaangalia chombo hicho, ninamtazamia Mungu na kile alichohidi.” Jambo ndilo hilo, inategemea kile unachoangalia, mahali imani yako ilipo. Sasa, kama chombo kikitangaza jambo hilo, huo ndio umbali tu unaoweza kwenda, kama imani yako iko kwenye hicho chombo.

⁷⁰ Kama vile maskini ndugu fulani wa thamani . . . Niliitwa, ni kama miaka kumi na mitano iliyopita, kumwombea mvulana akifa kwa dondakoo hili jeusi, alikuwa na ugonjwa wa moyo, nao walikuwa wamechukua kadiogramu, nayo ilionyesha ya kwamba moyo wake ulikuwa dhaifu kabisa, ninasahau huo mpigo ulikuwa nini, lakini alikuwa akienda.

Maskini mama na baba wakaniita kutoka mkutanoni, nao wakaketi kwenye vipandio kwa siku mbili ama tatu, na kusema, “Usipokuja . . .”

Nami nikasema, “Vema, mchukue mtu fulani.” Alisema ya kwamba . . . Nikasema, “Mungu anao watu Wake kila mahali.”

Akasema, “Lakini, Ndugu Branham,” kasema, “huelewi.” Nikasema . . . Kasema, “Naweza kulielezea?”

Nikasema, “Nitajaribu kulielewa.” Nami nikasema, “Nimechoka, wala si sawa kwangu kwenda mahali pamoja kama siwezi kwenda pengine.”

Akasema, “Lakini . . .”

Nikasema, “Isipokuwa Roho Mtakatifu aniambie niende.”

⁷¹ Akasema, “Lakini angalia,” akasema, “tumeketi kwenye mkutano huo kwa juma moja.” Kasema, “Tunajua ya kwamba haiwezekani, kwa kuwa watu wetu wenyewe katika ujirani wetu

wameketi katika mkutano huo, wa makanisa mbalimbali ya kimadhehebu, naye Roho Mtakatifu amewaambia la kufanya hasa, na jinsi ya kulifanya kutoka jukwaani, na imekuwa vile hasa Roho alivyosema.” Wakasema, “Ndugu Branham, tunajua ya kwamba usingeweza kufanya hivyo, kwamba haina budi kutoka kwa Mungu.” Kasema, “Kwa hiyo, utakuja na kumwomba mvulana wangu,” huyo baba mzee akasema, “atapata afya.”

⁷² Vema, aling’ang’ania, akashikilia sana. Kwa hiyo nikachukua koti langu na kuondoka, nikaenda hospitalini, ndipo daktari akakutana nami, naye akasema, “Nisingemsumbua,” kasema, “huyo mvulana huenda akafa dakika yoyote.” Naye daktari alikuwa mfuasi wa dhehebu lingine la kanisa, kwa sababu nilimhoji.

⁷³ Nikasema, “Lakini, Bwana, hu—huyo mvulana yuafa.” Nikasema, “Wewe ni Mkristo?” Akasema alikuwa mfuasi wa kanisa lingine, dhehebu *fulani*. Nikasema, “Vema, kama kasisi wenu angekuja, naye mvulana huyo awe wa dhehebu lile lile mnaloshiriki, na huyo kasisi alitaka kumfanyia desturi za ibada ya mwisho, ungemwachilia kasisi huyo aende?”

Akasema, “Bila shaka.”

⁷⁴ Nikasema, “Vema, kama . . . Baba huyu anaamini hilo, vivyo hivyo, kama ninaweza kumwomba mvulana huyo atapona, kama unavyoamini mvulana huyo angeokolewa, kama kasisi angemfanyia desturi za mwisho.” Ilinibidi kung’angaia kidogo, pia. Kwa hiyo akaniruhusu niingie, maskini huyo nesi akainua pua yake ndogo akarudi.

⁷⁵ Kwa hiyo tukapiga magoti kitandani, mvulana huyo alikuwa amepoteza fahamu. Kwa hiyo, nikaweka mikono yangu juu ya mvulana huyo na kuomba maneno machache tu ya maombi, nami nikasema, “Baba Mungu, sielewi, lakini maskini mzee huyu analia, naye aliniomba nije hapa. Na jambo pekee ninalojua kufanya ni kukuomba Wewe, nami,” kasema, “naomba ya kwamba utayaokoa maisha ya mvulana huyu, katika Jina la Bwana Yesu,” kisha nikasimama.

⁷⁶ Ndipo maskini huyo baba akamgeukia mama, akamkumbatia shingoni, nao wakaanza kukumbatiana na kupangusa machozi machoni mwao, na kusema, “Si ni ajabu, Mama?” Ndipo nikaangalia, naye maskini nesi huyo akageuza tu kichwa chake na kuangalia.

Kisha kasema, “Wazia jambo hilo yeye, Bob atapona. Loo, tunamsifu Bwana,” wakasema.

⁷⁷ Naye maskini huyo nesi . . . Wakanyoosha mkono juu ya mvulana huyo, na kunipa mikono, na kusema, “Asante, Ndugu Branham, kwa kumtii Bwana, kuja kuomba maombi ya imani kwa ajili ya mvulana wetu.” Kamwe sikusema zaidi ya maombi.

Ndipo yule nesi akasema, “Bwana, sidhani unaelewa.”

Akasema, “Loo, naam, ninaelewa.”

Kasema, “Unadai unampenda mvulana huyu.”

Kasema, “Bila shaka, tunampenda huyu mvulana.”

⁷⁸ “Vema,” kasema, “unaona . . .” Akasema . . . Akasema, “Unawezaje kutenda hivyo wakati huyu mvulana anakufa?” Kasema, “Sasa, katika historia yote ya matibabu wakati kitu *fulani* hiki,” sijui kilikuwa ni nini, “chombo kinaposhuka chini hivyo, mvulana huyo hawezi kupumua tena.” Kisha kasema, “Mnaona, mvulana huyo angeweza kufa dakika yoyote, moyo wake unadunda tu . . .” Ninasahau kupumua kwake, kulikuwa kubaya sana, nao moyo wake ulikuwa mbaya sana, alikuwa na vali wazi na kila kitu ndani yake, na moja ya vali ilikuwa imeziba ama chochote kile.

⁷⁹ Kisha kasema, “A—amepoteza fahamu sasa, hata yeye ni dhaifu sana hawezi kujua chochote.” Kisha kasema, “Halafu mnaweza kusimama hapo na kucheka na kupiga mayowe namna hiyo,” hakujua hayo yalikuwa ni makelele ya namna gani, “na kusema, kutenda hivyo na mwanao yuafa!”

⁸⁰ Ndipo maskini huyo muungwana, kamwe sitamsahau, akageuka na kuweka mkono wake, kama baba, juu ya mabega ya maskini msichana huyo mwenye umri wa kama miaka kumi na minane, maskini kipusa, mnajua hilo, unajua, maskini Annie, na kusema, “Sikiliza, mpenzi,” kasema, “unajua, unaangalia chombo hicho,” mnaona, kisha kasema, “hayo tu ndiyo unayojua, lakini,” kasema, “Ninaangalia ahadi katika Neno la Mungu.” Kasema, “Mvulana wangu ataishi, kwa kuwa Yeye alisema, ‘Maombi ya imani yatamwoko mgonjwa yule,’ na hayo yameombwa juu ya mvulana wangu.”

⁸¹ Vema, hiyo ni kama miaka kumi na mitano iliyopita, huyu mvulana ameoa na ana watoto wawili. Mnaona, kule kung’ang’ania, kwamba ataamini haidhuru chombo gani kinasema lolote. Imani yake haikuwa katika hicho chombo, ilikuwa katika ahadi ya Mungu.

⁸² Nuhu, baada ya kusikia ahadi ya Mungu, angeweza kung’ang’ania, kushikilia.

⁸³ Musa, alikuwa amemjua kiakili, kwa mama yake mtauwa, Dada yetu mpendwa Yokebedi, alikuwa amemsikia akifundisha kwa njia ya kiakili, jinsi ambavyo maisha yake yalikuwa yameokolewa kutoka kwa mamba, na jinsi ambavyo Mungu alikuwa amemfanya mtoto mzuri, naye alizaliwa kuwa mkombozi, na jinsi ambavyo Miriamu, dada yake, yule nabii mke, alikuwa amemfuata mpaka kwenye ufuo wa kuogelea, ambako binti Farao alikuwa akioga, na jinsi ambavyo Mungu alikuwa amemleta moja kwa moja na—na kumlelea mumo

humo katika ikulu ya Farao, na jinsi ambavyo alikuwa anaenda kuwakomboa watoto.

⁸⁴ Sasa, kiakili alijua jambo hilo. Lakini, mnaona, kosa dogo la kwanza . . . Loo, msilikose, enyi kanisa. Huenda ukalijua kwa msimamo wa Neno, huenda ukajua ya kwamba Biblia ilisema kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa huyo, bali wewe omba mpaka Mungu aseme maombi ya imani yanakuokoa *wewe*. Hiyo ndiyo tofauti.

⁸⁵ Musa alijua kiakili kwamba yeye alikuwa ndiye mkombozi, lakini alipowazia watoto wa Mungu wangemwelewa hapo alipomwua yule Mmisri, uvumi mdogo wa kwanza ulipotokea, hakuwa mvumilivu hata kidogo. Kabla tu hata haujamfikia Farao, alikimbilia jangwani, kwa sababu hakuwa mvumilivu, hakuwa na hakika sana, alijua hilo tu kwa msimamo wa Neno, ile ahadi.

⁸⁶ Lakini siku moja aliona kichaka kilichokuwa kinawaka moto, nacho kilikuwa kinawaka, wala hakikuteketea. Kwa hiyo Musa akachukua, akapanda mlimani, nayo ile Nguzo kubwa ya Moto iliyokuwa imwongoze siku zake zote zilizosalia ilikuwa huko nyuma kichakani. Na katika Nguzo hii ya Moto Sauti ikanena, “Nimeyaona mateso ya watu Wangu, nimesikia kuugua kwao; nami ninakumbuka ahadi Yangu kwa Ibrahimu, nami nimeshuka kuwakomboa. Sasa, shuka uende kule.”

⁸⁷ Sasa, nena kuhusu kung’ang’ania! Akaenda moja kwa moja mbele ya Farao, akasema, “Waache waende!” Kwa nini? Alikuwa amezungumza uso kwa uso na Mungu mpaka akatimiza agizo lake.

⁸⁸ Nafikiri kama ndugu wahudumu siku hizi wasingelichukua tu kutoka kwenye msimamo wa kiakili, lakini wangejitafutia mahali fulani upande wa nyuma ya jangwa kwenye mchanga huo mtakatifu, ambapo Shetani hawezi kuweka miguu yake michafu ya kutokuamini, na kukaa hapo mpaka ujumbe utakapotoka kwa Mungu na kukuweka mahali pako, kukuweka katika huduma, ndipo pepo wote kutoka katika mateso wasingeweza kukutikisa kwake, unajua umeitwa.

⁸⁹ Nafikiri kila Mkristo anapaswa kufanya hivyo, kabla hujatoka na kumkiri Roho Mtakatifu, kukiri kwamba una ubatizo, kunapaswa kuwe na mawasiliano kama hayo ya kibinafsi na Mungu mpaka wasomi wote ulimwenguni wasingeweza kulielezea likuondokee. Unajua, umekuwa huko, umekuwa na shahidi, unajua ndivyo ilivyo.

⁹⁰ Hayo ndiyo masharti. Yesu aliwaambia wanafunzi, “Ninyi ngojeni, mnajua ile sehemu ya kiakili, mnajua Neno, bali ninyi ngojeni huko juu kwenye mji wa Yerusalemu, mpaka mtakapovikwa Nguvu zitokazo Juu.” Ndipo wakajua.

⁹¹ Loo, jamani! Jinsi maskini Daudi, huko nyuma kabisa upande wa nyuma ya jangwa, maskini jamaa mwekundu,

mwenye mabega yaliyoinama akiwachunga kondoo wake huko nje kwa ajili ya baba yake, siku moja dubu aliingia na kumchukua mwana-kondoo, naye akamfuata, na kuchukua kombeo lake dogo na kumwua huyo dubu!

⁹² Halafu tena, simba akaingia na kumchukua mmoja, naye akatoka mbio pamoja na huyo mwana-kondoo. Na yule, maskini Daudi, huyo alikuwa ni kondoo wa baba yake, naye akamfuata kwa kombeo dogo, si kwa bunduki kubwa sasa, kwa kombeo lenye jiwe ndani yake, bali tumaini lake lilikuwa kwa Mungu. Akalitupa hilo jiwe, akampiga simba, akamwangusha chini, ndipo simba alipoinuka, akamwua, akamrudisha huyo kondoo. Yeye alishikilia, kwa sababu, kwa nini? Alikuwa na wajibu kwa ajili ya kondoo wa baba yake.

⁹³ Nafikiri hiyo inapaswa kuwa ni hisia ya kila kasisi, tuna wajibu kutoka kwa Mungu kwa ajili ya kondoo wa Baba. Ibilisi wa kale wa maradhi ameingia miongoni mweni Wakristo; anajaribu kuwaondosha. Mimi, bila elimu, si—si—sijui lolote kuhusu tiba, bali kitu pekee nilicho nacho ni kombeo hili dogo la maombi, ninawajia usiku wa leo, nataka kuwarudisha. Aliahidi maombi ya imani yatamwokoja mgonjwa huyo.

⁹⁴ Labda wale watu mashuhuri wa kielimu, zile dawa mashuhuri za kisayansi na kadhalika, huenda wakayacheka, sijui lolote kuhusu hilo, kama vile Daudi, wakati alipojaribu kuchukua upanga na kuvaa koti la kikanisa la Sauli, halikumwenea. Kamwe halimwenei mtu halisi wa Mungu. Lakini akalichukua, akasema, “Hebu niende na kile nilichothibitisha.”

⁹⁵ Hicho ndicho kitu pekee nijuacho, Wakristo, ni kwenda na kile ambacho nimethibitisha kuwa ni Kweli, hilo ni Neno la Mungu, Neno Lake, likisimama papo hapo. Kuwafuatilia watoto Wake wagonjwa, hebu na tuwarudishe kwenye malisho ya kijani kibichi yenye kivuli, na maji matulivu, na afya njema, nguvu.

⁹⁶ Maskini Samsoni akisimama pale nje, na kunaswa, kama tulivyonena habari zake hivi majuzi usiku, huku Wafilisti wamemzunguka, hakuwa na kitu ila mfupa wa taya la nyumbu, lakini wakati angeweza kunyosha mkono na kugusa maskini hivyo vishungi saba, aling'ang'ania sana.

⁹⁷ Shamgari, watu wengi hawakusoma habari zake katika Biblia, alikuwa mmoja wa waamuzi wa Israeli. Aya moja tu ndogo iliandikwa juu yake, katika Biblia nzima. Lakini alipokuwa amesimama pale, baada ya kumaliza kuvuna, watoto wake wadogo walionekana wamekonda na maskini, mke wake, labda mikono ya nguo imetokeza nguoni mwake, hao Wafilisti wangeingia moja kwa moja, wachukue kila kitu walichokuwa nacho mara tu baada ya kukishughulikia sana. Wakayaweka mahali pazuri, ndipo Wafilisti wangeingia na kuwanyang'anya.

98 Kwa hiyo mnamo wakati alipozipura nafaka huko ghalani, aliwazia, “Vema, labda tunaweza kuishi, nami ninaweza kuuza baadhi yake, na kuwanunulia wasichana wangu nguo chache, na viatu kwa ajili ya mvulana wangu, na labda niweze kumnunulia mke wangu nguo ya bei rahisi mwaka huu,” ndipo akasikia kitu fulani, akavuta nyuma dirisha la mlango wa ghala na kuangalia huko nje, mlango wa ghala, hasa, na kuangalia nje. Hawa hapa Wafilisti elfu moja wanakuja, silaha, mikuki, panga, watu waliofunzwa, *pump, pump*, wanapanda, moja kwa moja kwenye barabara kuu, hapo wangebeba nafaka yake.

99 Akasimama pale. Sasa, yeye hakuwa mpiganaji, alikuwa ni mkulima, hata hakuwa na upanga, tujuavyo sisi, lakini ilitokea kwamba alikumbuka, “Mimi ni Myahudi na nimetahiriwa, mimi ni mtoto wa Mungu, nina haki. Nina njia ya kumfikia Mungu yeye yule wa Daudi, nina njia ya kumfikia Mungu yeye yule wa Musa, Mimi, nina njia ya kumfikia Mungu yeye yule wa Danieli.” Naye, Roho akashuka juu yake, naye akashika hilo konzo la maksai, akatoka akaenda kule, na kung’ang’ania, ndipo akawaua Wafilisti elfu moja kwa konzo la ng’ombe, fimbo, kile wanachompigapiga maksai nacho, akawaua Wafilisti elfu moja.

100 Nilikuwa, wakati mmoja, nikienda kwenye uwanja wa michezo ambamo nilikuwa nihubiri, basi kulikuwa na uwanja mkubwa wa watu, maelfu mengi, wakingojea. Nami nikasoma kitu fulani kidogo juu ya uwanja huo, daima kilininii, ulikuwa ni uwanja wa kandanda, daima kilinitia moyo. Kulikuwa na ubao mdogo pale, uliosema, “Si ukubwa wa mbwa katika pambano, bali ni ukubwa wa pambano lililoko ndani ya huyo mbwa.” Kwa hiyo nafikiri hilo ndilo jambo lenyewe, ni kuwapata Wakristo halisi wengi waling’ang’anie. “Mungu alilahidi hilo, na ni langu!” Kweli.

101 Yohana Mbatizaji aling’ang’ania sana. Wangesema, labda Kayafa, ama baadhi ya makuhani wangejitokeza na kusema, “Huyu hapa Kasisi, Dk., Ph.D. *Nanii*. Je, hufikirii anafaa kuwa Masihii?”

Yohana akasema, “Siye.”

Wakamleta mwingine, “Huyu hapa mtu mwema. Naye je?”

“Huyo siye,” kwa kuwa alijua wakati atakapomwona Hua huyo akishuka kutoka Mbinguni, huyo angekuwa ni Yeye, basi akashikilia.

Loo, ni mengi sana katika Biblia ya kuzungumzia, kamwe nisingeweza kuyafikia.

102 Hebu tumwendee yule mwanamke Myunani. Kwanza, yeye alikuwa Myunani, hakuwa Myahudi, alikuwa Mmataifa, bali alikuwa amesikia sifa za Yesu, alikuwa amesikia habari za wakosoaji pia, jinsi walivyomkosoa; lakini hakuwajali wakosoaji, alikuwa akisikiliza ule umaarufu.

103 Yeye, akiwa Myunani...Mwajua, daima una kitu cha kuzuia. Lakini unajua, kwa *njia moja au nyingine*, imani hupata chanzo ambacho watu hawakioni. Imani hupata chanzo chake, watu hawaoni hilo. Kwa hiyo hapana shaka ndivyo ilivyokuwa kwa maskini mwanamke huyu, kwamba imani ilikuwa imepata chanzo. “Neno la Mungu,” Biblia ilisema katika Waebrania 4:12, “ni Upanga,” ni Upanga, “unakata mafuta kwenye mfupa, kugawanya, kwa roho, na ni Mtambuzi wa mawazo na makusudi ya moyo.” Hivyo ndivyo Neno lilivyo.

104 Hiyo ndiyo sababu Yesu angeweza kutambua kilichokuwa katika mawazo ya watu, kwa sababu Yeye alikuwa ni Neno. Na kama Neno likikaa ndani yako, basi si wewe, Neno ndilo linalotoka na kupambanua. Na kuna kitu kimoja tu kinachoweza kushughulikia Hilo, Neno hilo. Si elimu, nitawahakikishia hilo. Imani ndicho kitu pekee kinachoweza kuutumia upanga huo wa imani. Kama nilivyosema hivi majuzi usiku, imani katika Neno la Mungu itatoboa tundu katika ugumu wowote, bali huna budi kuliadini.

105 Alikuwa na vizuizi vingi, alikuwa navyo mwenyewe, bali imani yake haikuwa na vizuizi vyovyote. La, imani haina kizuizi chochote, imani huamini tu. Haina kizuizi hata kidogo, tayari umepita kizuizi cha sauti, kama vile yule mama alivyokuwa akizungumzia. Imani haina kizuizi, unaweza kuwa nacho, bali imani yako haina. Imani yako haina kizuizi hata kidogo.

106 Huenda yeye...Huenda walimwambia, “Wewe ni Myunani, hupaswi kwenda kule, huyo ni Myahudi. Huyo ni Myahudi ambaye wanadai mambo haya yote kumhusu, wewe ni Myunani.”

107 Lakini, mnaona, walikuwa wakijaribu kuwa na kizuizi cha jamii pale, lakini imani haijui kizuizi cha jamii, haikijui kabisa, la, maana huenda aliwazia hili: “Kama Yeye ni Yule ninayeamini kuwa Ndiye, Yeye ni Mungu, na kama Yeye ni Mungu, Yeye ndiye Muumba wa kila kiumbe. Endapo Yeye ni Mungu kamwe, Yeye ni Mungu wa viumbe vyote, na iwapo Yeye si Mungu wa viumbe vyote, basi Yeye si Mungu.” Hiyo ni njia nzuri ya kuliangalia.

108 Vema, haidhuru kama alikuwa Myunani, angali aling'ang'ania, alikuwa na subira. Ndipo huenda mtu fulani alikuja na methali hii ya kale, mwajua, kama ile wangali nayo siku hizi, “Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama hicho.” Lakini haidhuru ni wangapi waliompigia makelele, “Siku za miujiza zimepita,” angali alishikilia. Huenda hilo lilikuwa ni kwa ajili ya hao walioliamini, bali si kwa ajili yake, jambo fulani lilikuwa tayari limetendeka ndani ambalo lilimjulisha ya kwamba hazikuwa zimepita.

109 Na mpaka utakapovuka kizuizi hicho, kamwe hutafaa chochote. Huna budi kupita kizuizi hicho, “Mungu alikuwako, bali hayuko sasa,” Yeye angali ni Mungu kama aliwahi kuwa

Mungu. Na kama Yeye si Mungu yeye yule leo, Yeye kamwe hakuwa Mungu. Mnaona? Jambo ndilo hilo. Ni, mwanadamu alipoteza imani yake, si Mungu aliyepoteza nguvu Zake, Mungu akaighairi ahadi Yake; ni, mwanadamu alighairi ahadi ya kuamini.

¹¹⁰ Bado aling'ang'ania. Kama siku za miujiza zilikuwa zimepita kwa hao wote, hazikupita kwake. Kwa nini? Alikuwa amekipita kizuizi hicho cha sauti. Alishikilia kitu fulani, kitu fulani kilikuwa kimemgusa.

¹¹¹ Vema, daima kuna kundi lingine kwa maskini mama kama huyo. Baadhi yao huenda walisema, "Unajua nini? Mumeo ni mfanyabiashara, yeye ni mfuasi wa kanisa kubwa upande *huu*, na kama ukishuka kwenda *kule* kwenye kundi hilo, mume wako atakuacha." Sasa, hicho ni kizuizi kikubwa sana kupita, lakini nakwambia, kama ukipata kushikilia imani kama yeye alivyofanya, hilo halitaleta tofauti yoyote. Uh-huh. Sawa. Hilo halikuleta tofauti yoyote kwake, iwe ni mume ama si mume, alikuwa njiani kwenda kumlaki Yesu. Mnaona? Aling'ang'ania.

¹¹² Halafu huenda kulikuwa na kundi ambalo daima husimama karibu, linasema, "Lakini ngoja kidogo, ukishuka kwenda kule, Lydia," vyovyote jina lake livyokuwa, "unajua, utakuwa kitu cha kuchekwa kwa taifa letu, kwa sababu unajua hakuna kitu kama hicho huko chini, nawe unajua hiyo ni hadithi tu ya uongo ya Kiyahudi. Wamekuwa na upuuzi kama huo wote, lakini, tumesikia habari zake, bali si kitu ila methali tu, wimbo wanaouimba." Mwajua, wangali wana kundi hilo. Naam. Kwa hiyo, lakini alipofika kwenye kundi hilo, angekuwa ni kitu cha kuchekwa, na kadhalika, alikuwa mvumilivu sana, akawapita moja kwa moja.

¹¹³ Vema. Ndipo likaja kundi la wahudumu. Loo, jamani! Hilo ni baya kupita. "Sasa, angalia hapa..." Nimemwita Lydia, natumaini hakuna Lydia hapa, lakini huenda ikawa ni sawa. Natumaini una imani ile ile aliyokuwa nayo. Kwa hiyo basi, wakati Lydia alipofika kwenye shirika la wahudumu wao walisema, "Jambo moja kwake, unajua wewe ni mfuasi hapa juu wa kanisa letu, na hilo ni la Kipentekoste..." ama namna fulani ya kundi kule chini, mwajua. Hata hivyo, kasema, "Ukishuka kwenda kule, tutakupua kumbukumbu ya kanisa lako, barua yako, tutakuondoa moja kwa moja kwenye kitabu. Sisi... Huwezi kurudi kanisani tena. Tutakuondosha tu, nawe utakuwa mtu wa kuchekwa, mume wako atakutaliki, naye ataoa mwanamke mwenye sura nzuri kuliko wewe," na mambo haya yote.

¹¹⁴ Lakini hilo halikumkomesha hata kidogo, barua ya kanisa ama chochote kile hakikumkomesha. Kwa nini? Alikuwa amesikia. "Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno la

Mungu.” Aling’angania, alijipenyeza moja kwa moja kupitia kila kizuizi.

115 Sasa, anamfikia Yesu. Sasa, yeye aliwazia, “Yote yamekwisha sasa.” Hivyo ndivyo watu wengine wanavyofikiri wanapompokea Roho Mtakatifu, “Yote yamekwisha.” Ni mwanzo tu, mnaona, hapo ndipo unapohitaji kun’ang’ania, utakapofika.

116 Alipofika kwa Yesu, Yesu alisema, akamtetemesha kwelikweli. Ninaamini Yeye alijua alikuwa anakuja. Kwa hiyo, alipofika, Yeye alimgeukia na kumjulisha ya kwamba Yeye hakutumwa kwa jamii yake. Loo, jamani, hilo lingekuwa ni sikitiko la jinsi gani!

117 Loo, lakini ilifanya nini? Hilo halikumkomesha hata kidogo, hata kidogo, bado alimwita Mwana wa Daudi. Bila shaka, Mmataifa hana mamlaka juu ya Kristo kwa jina la Mwana wa Daudi. La, la. Mnaona, Mwana wa Daudi alikuwa chini ya Ufalme, naye Kristo ni Mfalme wa Wayahudi. Lakini kwa Kanisa, Yeye si Mfalme, Yeye ni Bwana, amina, Yeye ni Mume, kama vile Sara alivyomwita Ibrahimu bwana wake. Yeye ni Bwana wa Kanisa, bali ni Mfalme wa jamii ya Kiyahudi.

118 Kwa hiyo wakati alipomwabudu na kusema, “Bwana, nisaidie,” Yesu alisema, “Lakini unajua, si vema Kwangu kukitwaa chakula cha watoto, na kuwatupia ninyi mbwa.”

119 Loo, jamani! Kama huyo angalikuwa ni Mpentekoste wa kisasa, angeinua maskini pua hiyo na kusema, “Sitahudhuria mkutano kama huo tena.” Kwa nini? Hawana kushikilia alikokuwa nako. Hiyo ni kweli. Alikuwa ameshikilia, alikuwa amesikia, na imani ilikuwa imeshika. Alikuwa na sababu, alikuwa na haja, naye kamwe hangeachilia. Hiyo ni kweli. Ninapenda hilo. Naam, bwana. Angali alishikilia, ingawa aliitwa mbwa, na jamii iliyokuwa duni kuliko mbwa.

Kasema, “Sijatumwa kwa jamii yako. Nimetumwa tu kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli.”

Naye akasema, “Bwana, nisaidie.”

Akasema, “Si vema kwangu kukitwaa chakula cha watoto na kuwatupia mbwa.” Loo, jamani!

120 Yeye hakuwa mmea wa tuta, ambaye hana budi kubembelezwa. La, la. La, la. Yeye hakuwa mmea wa tuta, ambaye hana budi kubembelezwa. Yeye hakuwa chotara wa kisasa, *anayejiita* mwaminio, wa zao la siku hizi. Alikuwa ameshikilia kitu fulani. Sio, “Vema, mimi ni Mmethodisti, wala si lazima nichukue hilo.” “Mungu abarikiwe, mimi ni mfuasi wa Assemblies.” “Mimi ni mfuasi wa Church of God, si lazima nichukue hilo.” La, la. Huo ni aina ya uhotara, umezaliwa katika madhehebu fulani. Lakini Mkristo halisi wa kweli, ukoo

safi amezaliwa kwa Neno la Mungu na kushikilia, haidhuru ni kitu gani kinachotukia.

¹²¹ Kitu chochote kinachoonekana kuwa bubu kwangu ni nyumbu. Nyumbu hajui alikotoka. Yeye si nyumbu, wala si farasi, yeye ni mchanganyiko kati ya nyumbu na farasi. Yeye si mpole, ni katili, ni duni, atangojea maisha yake yote apate, kukupiga teke kabla tu hajafa. Unaweza kumwita, atayanyoosha tu hayo masikio makubwa juu, “Hoo, hoo.” Mnaona? Yeye hajui. Hiyo ni kweli. Yeye ni chotara.

¹²² Hiyo ndiyo shida ya kanisa siku hizi, machotara wengi kupita kiasi *wanaojiita* Wakristo. Vema. Wanainua masikio yao juu, wanasema, “Hoo, siku za miujiza zimepita. Hoo, hoo.” Hujui kama wewe ni Mkristo au mwenye dhambi, hujui kama wewe ni mwaminio au asiyeamini. Chotara!

¹²³ Chochote kilicho chotara kiko nje ya barabara halisi, iliyo kuu, iliyoandaliwa. Inatupasa kuwa na wakati kidogo, tuzungumze juu ya *Mbegu ya Asili*, tuone inakotoka. Chotara, hajui mahali pake, hajui baba yake alikuwa ni nani, mama yake alikuwa nani, ama chochote kile. La, yeye hajui, hana ukoo safi, hawezi kuwa na ukoo safi. Kamwe hawezi kujizaa mwenyewe.

¹²⁴ Hiyo ndiyo shida ya makanisa siku hizi, hayawezi kujizaa tena. Wao ni chotara, hawajui kama wao ni wa Mungu, ama dhehebu fulani. Kitu pekee wanachoweza kutoa ni mfuasi, si Mkristo. Haleluya! Mimi, labda sikupaswa kusema hivyo, lilikuwa tayari limesemwa. Hiyo ni kweli. Hajui yeye ni wa nini, anajua tu yeye ni Mmethodisti, Mbaptisti, ama Mpentekoste, hayo tu ndiyo ajuayo.

¹²⁵ Lakini loo, jinsi wa ukoo safi alivyo mzuri! Loo, jamani! Anaweza kukwambia baba yake alikuwa ni nani, mama yake alikuwa ni nani, babu yake, na nyanya yake, na mama wa nyanya yake, na huko nyuma kabisa, yeye anajua. Yeye ni mpole, mwema, unaweza kuzungumza naye, anasikiliza, anaweka kichwa chake begani mwako, amejaa upendo. Kwa nini? Yeye ni ukoo safi.

¹²⁶ Vivyo hivyo na Mkristo wa ukoo safi aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu. Hawaingii katika mabishano yoyote ya kimadhehebu, wanajua Baba yao ni Nani, wanajua walikotoka, wanajua mahali Roho alikotoka, wanajua wamezaliwa na Nani. Hawabishanii kanuni zenu za imani. Unaweza kuzungumza nao kuhusu upendo, kuhusu uponyaji wa Kiungu, mambo haya yote kwa sababu wamezaliwa na Mungu. Kung’ang’ania? Ninapaswa kusema! Haikulazimu kuwapiga, watauvuta mzigo kwa vovyote vile. Hiyo ni kweli. Loo, jamani! Ni ajabu jinsi gani!

¹²⁷ Wakristo chotara, hilo ndilo zao siku hizi; si yeye, la, bwana. Angalia, wakati Yesu aliposema, “Sijatumwa kwa jamii yenu,” akimpa jaribio. . . . Alikuwa na wakati mgumu sana kumwendea,

lakini alipofika Kwake, basi alivunjika moyo, “Sijatumwa kwa jamii yenu.”

Lakini wakati aliposema, “Bwana, nisaidie,” Yeye alisema, “Si vema Kwangu kukitwaa chakula cha watoto, na kuwatupia mbwa.”

Sikilizeni hili: “Bwana, hiyo ni kweli.” Loo, jamani! Imani daima itakubali Neno kuwa kweli. Um-hum. Naam, bwana. “Ni kweli, Bwana, lakini ninataka tu makombo.”

¹²⁸ Huyu si mwaminio mamboleo siku hizi, “Utashuka uje moja kwa moja na ufanye jinsi ninavyokutaka Wewe ufanye, la sivyo si—si—si—sitalipokea.” Naam. Hivyo ndivyo Naamani alivyokuwa, akijaribu kuuondoa ukoma wake; bali huna budi kulichukua jinsi anavyolileta. Basi wakati imani inapolishikilia, utaendelea nalo, naam.

¹²⁹ Alikuwa tu akitafuta makombo. Kumbukeni, mwanamke huyu hakuwa amewahi kuona mwujiza, alikuwa ni Myunani, bali aliamini kwa vyovyote vile. Alikuwa kama yule kahaba, Rahabu.

¹³⁰ Yule kahaba, Rahabu, *aliposikia*, wakati alipowaficha wale wapelelezi, alikuwa ni Mmataifa, aliyetengwa na jamii, kahaba, bali alisikia, hakusema, “Mleteni Yoshua hapa juu na mniache nimwangelie. Hebu nione jinsi alivyo mrefu, jinsi alivyo na sura nzuri, jinsi anavyochana nywele zake, jinsi anavyojipamba, jinsi alivyo mkubwa, jinsi alivyo na mabega makubwa.” Hakujali alionekana je, alisema, “*Nimesikia* yale Mungu aliyowafanyia.” Haya basi. “Sijali jinsi Yoshua anavyoonekana. Sijali kama ana Ph.D., ama LL.D., ama hana chochote. Ninajua Mungu yu pamoja nanyi, nami nataka ulinzi.” Amina.

¹³¹ Sijali kama wanawaita watakatifu wanaojifingirisha, walokole wa Kipentekoste, Full Gospel, chochote kile, ninamtaka Mungu. Ninataka neema Yake, nataka nguvu Zake, nataka upendo Wake, nataka msamaha Wake. Sijali itabidi uitwe nini. Si lazima nione *hili*, *lile*, ama *linginelo*, kama Yeye ni mkubwa ama mdogo, ama chochote alichu, ni—ninataka tu kumwona. Ninataka kuwa pamoja na neema na rehema Yake; hilo ndilo tunalohitaji.

¹³² Angalieni, mwanamke huyu alikuwa na mtazamo mzuri kwa karama ya Mungu. Jinsi ilivyokuwa tofauti kwa hao Mafarisayo! Jinsi ilivyokuwa kwa hao Wayahudi, watawala, walisema, “Sisi tunataka kuona mwujiza kutoka kwako,” loo, upande wa kikanisa!

¹³³ Lakini maskini Mmataifa huyu mdogo, asiye na elimu, alisema, “Ninii tu, Bwana, ninataka tu makombo.” Kasema, “Ni—ninii... Unajua mbwa hula makombo yanayoanguka kutoka kwa meza ya bwana, hayo tu ndiyo ninayoomba.”

¹³⁴ Hakusema, “Inakubidi kushuka nyumbani kwangu na kuweka mikono Yako juu ya mtoto wangu.” Yeye hakusema, “Kama utashuka na kunena katika lugha nyingine huko nje, na kuniambia yote kulihusu, ni—ni—nitaamini.”

¹³⁵ Alisema, “Ninataka tu makombo, yaangukayo tu, ndiyo yote ninayotafuta.” Mnaona, alikuwa na mtazamo mzuri, alikuwa na mtazamo mzuri kwa karama ya Mungu. Alikuwa ndiye Mmataifa wa kwanza ambaye Yesu aliwahi kumfanyia mwujiza, Mmataifa wa kwanza. Imani daima hukubali kwamba Neno ni kweli, nayo imani daima hutenda kazi kwa unyenyekevu. Imani daima hukubali Neno kuwa kweli, na daima hutenda kwa unyenyekevu.

¹³⁶ Waangalieni Martha na Mariamu, wakati maskini Martha alipokuwa amedhihakiwa sana, ama, amenenwa sana kuhusu kuidumisha nyumba safi, lakini wakati Lazaro alipokufa alimwendea. Angalia jinsi alivyong’ang’ania, kung’angania: Ilimbidi kupita kwenye wakosoaji wote waliosema, “Yuko wapi yule mhubiri mtakatifu anayejibingirisha aliyekuwa hapa, aliyedai alimpenda ndugu yako *sana?*” Mnaona?

¹³⁷ Yesu alijua, Baba alikuwa amemwambia, “Nenda zako ukangoje mpaka Lazaro atakapokufa, nami nitakurudisha Wewe,” maana Yeye alisema hivyo, alisema hakufanya lolote mpaka amwone Baba akimwonyesha kwanza. Hiyo ni kweli.

¹³⁸ Kwa hiyo akaondoka, nao wakaagizia aitwe, wala hakuja, nawazia alichekwa wakati huo, “Yuko wapi? Uh-huh, akakimbia.” Kisha akaagizia tena, Naye akakimbia tena, akaenda kwenye mji mwingine.

Ndipo, hatimaye, akageuka, akawaambia wanafunzi Wake, “Lazaro amelala.”

Kasema, “Vema, anafanya vema.”

Kasema, “Amekufa. Na kwa ajili yenu, nina furaha sikuwapo. Lakini nitaenda nikamwamshe.”

¹³⁹ Lakini maskini Martha hakumsikia akisema hivyo. Huyu hapa anakuja, aking’ang’ania, akasema, “Bwana, kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa. Lakini, hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa.” Ninapenda hilo. Loo, ninapenda hilo! “Hata sasa, hata sasa!”

Huenda ukasema, “Ndugu Branham, daktari aliniambia mimi. . .”

“Lakini, hata sasa!”

“Nimekuwa mgonjwa kwa miaka arobaini.”

“Lakini, hata sasa, Bwana!” Loo, jamani!

“Nimekuwa nikimtafuta Roho Mtakatifu kwa muda mrefu. Lakini, hata sasa, Bwana, wakati nikiwa Mbele Zako!”

140 “Lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa.” Naye akageuka bila kuhimizwa sana. Mnaona, Yeye hukujaribu, aone unavyoshikilia, usikate tamaa. Na kama imani kweli ikishikilia, haitakata tamaa. Kasema, “Hata sasa, Bwana, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa.”

Yesu akageuka na kusema, “Naam, Martha,” kasema, “ndugu yako atafufuka katika ufufuo. Atafufuka katika siku ya mwisho.”

Kasema, “Naam, Bwana, alikuwa mvulana mzuri, ninajua alikuwa mvulana mzuri, mimi . . . yote hayo ninaamini.”

141 Yesu akasema, “Mimi *ndimi* Ufufuo na Uzima; yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, ataishi. Kila aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe. Unasadiki haya?” A-ha, sasa, hilo lilimpa nini?

142 Sasa, alikuwa na haki ya kumkemea, na kusema, “Kwa nini Wewe hukuja? Nilikuita. Niliacha kanisa langu, nikaacha dhehebu langu, nikawaacha marafiki zangu, nikaacha karamu ya karata, sikuenda kwenye mchezo wa karata tena, niliua, kila kitu. Nikaja, nikikuamini Wewe.” Kumbukeni Roho Mtakatifu hakuwa amekuja bado sasa, kuwafundisha vinginevyo.

143 Lakini akasema, “Niliacha kila kitu, na kukufuata Wewe, na nilipokuhitaji Wewe, hukuja. Nilipoagizia, Wewe ulinipuuza na kuendelea; nikaagizia tena, na Wewe ukanipuuza.” Ilionekana kana kwamba angeweza kubishana Naye, bali alisahau yote kuhusu hilo. Alitaka kumfikia, hiyo ndiyo sababu alipata alichoomba.

144 Kama yule mwanamke Mshunami mbele ya Eliya, yeye aling'ang'ania, akaja na kuanguka miguuni pake, naye akasema. . . Eliya alisema, akisha kujua shida yake ilikuwa ni nini, alimwambia Gehazi, akasema, “Chukua fimbo yangu, nenda, uiweke juu ya huyo mtoto mchanga.” Naye akajifunga viuno vyake akaenda zake.

145 Lakini aling'ang'ania, imani yake haikuwa kwenye ile fimbo, ilikuwa katika huyo nabii, naye akasema, “Kama Bwana Mungu aishivyo, na nafsi yako haifi kamwe, sitakuacha.” Alishikilia, asingeweza kuliondokea, kwa hiyo akajifunga viuno vyake na kuondoka. Amina. Hivyo ndivyo ilivyo.

146 Kama yule mwanamke Mshunami angeweza kuwa na imani kama hiyo katika nabii, kama Martha alikuwa na imani kama hiyo katika Yesu, vipi siku hizi wakati tuna miaka elfu mbili ya miujiza ikimiminika daima? Wakati kote ulimwenguni, na usiku kucha, saa ishirini na nne, watu wanaponywa na kujazwa na Roho Mtakatifu ulimwenguni kote, miujiza ya kuponya na kuwafufua wafu, na kutoa pepo, hivi hatuwezi kung'ang'ania kulishikilia Neno la Mungu, tukijua Yeye hana upendeleo,

kushikilia pale, kung'ang'ania mpaka atakapokuja? Hakika, kung'ang'ania, bila shaka.

¹⁴⁷ Kama vile yule mwanamke, alishuka akaja maskanini yapata miaka mitatu iliyopita; nilikuwa mle ndani kwa usiku mmoja. Mwanamke fulani alikuwa mle ndani, alikuwa na uvimbe wenye uzito wa ratili hamsini, alikuwa amevimba namna *hii*. Huenda mwanamke huyo yuko hapa usiku wa leo. Nikaingia kupitia mlango wa nyuma, na kuingia kwenye maskini maskani ya kale pale, nami nilikuwa nikihubiri. Na kwa hiyo nikageuka na kurudi. Alikuwa ametoka California, wala asingeweza kutembea, naye aling'ang'ania hata hivyo. Wao walisema mimi . . . Akasema, "Nimekuja Ndugu Branham apate kuniombea."

Ndipo baadhi ya wazee wanasema, "Alitangaza ya kwamba hatawaombea wagonjwa usiku wa leo."

Akasema, "Anatokea upande gani?" Si mimi, yeye alimwamini Mungu.

¹⁴⁸ Kwa hiyo wawili wa hao wazee wa kanisa, ama watatu, wakamchukua mama huyu mkubwa, mnene, na kumbeba hadi kwenye mlango mdogo ninaotokea nyuma ya maskani, bila mimi kujua alikuwa pale apate kuombewa, nami nikamaliza kuhubiri, nikaanza kutoka nje, naye akanishika kwenye mguu wa suruali, naye akashikilia pale, akasema, "Ndugu Branham, sitachukua wakati wako kuniombea, bali niwekee tu mikono yako." Jambo ndilo hilo. Alikuwa amedhamiria.

¹⁴⁹ Yapata miezi sita ama minane baadaye . . . Yule mama aliyesimama pale usiku huo alikuwa amevimba namna *hiyo*, madaktari wasingemgusa kwa chochote kile.

¹⁵⁰ Amerudi kwenye mikutano yangu kote California, atakuwa huko tena sasa, amekua maskanini tangu wakati huo, ni waziwazi tu kama nilivyo mimi, ndipo kasema, "Yeyote wa hao wanawake anaweza kuja, anichunguze, hakuna alama ya kisu juu yangu, kitu hicho kiliniacha." Kwa nini? Aling'ang'ania. Amina. Imani yake ilikuwa imara.

Imani yangu haijajengwa juu ya chochote
pungufu

Ila Damu ya Yesu pamoja na haki;

Wakati yote yaliyoizunguka nafsi yangu
yakiondoka,

Basi Yeye ndiye tumaini langu na ngome yangu
yote.

Kwa kuwa juu ya Kristo, mwamba imara,
ninasimama;

Ardhi zingine zote ni mchanga udidimiao.

¹⁵¹ Kung'ang'ania, imani yao ilikuwa imeshikilia Neno Lake wala haingeachilia.

152 Kama vile Mikaya alivyokuwa kule chini mbele ya Ahabu na Yehoshafati. Kulikuwa na hamsini, ama, la, mia nne, nadhani, watu wazuri waliostaarabika walitokea, waliolishwa vizuri, wamevalishwa, manabii wa Ahabu. Walitokea wakitabiri, Yehoshafati, akiwa ni mtu mwenye haki, kulikuwa na kitu ambacho hakikukolea vizuri, mnaona, hakuwa na imani.

153 Hao jamaa wote wakisimama pale, seminari nzima ilikuwa huko nje, na kusema, "Angalia hapa, kwea, Ahabu," kwa sababu walikuwa wakiamua, "nchi hiyo ni mali yako, Ramoth-gileadi, ni yako, kwa hiyo ni yako. Kwea ukaiteke, Bwana yu pamoja nawe."

Zedekia alikuwa na seti kubwa mno ya pembe, namna *hii*, akasema, "Kwa hizi utawasukuma kote kote watoke nchini."

Yehoshafati akaangalia kote, akaona hakukuwa na imani, "Haidhuru," akasema, "hapa," akasema, "hivi huna mwingine?"

154 Akasema, "Ati mwingine? Kuna mia nne walio bora kuliko wote. Wameelimishwa, wamefunzwa, ni watu wa Mungu." Lakini mnaona, hapakuwapo na imani pale.

Akasema, "Hakika, unapaswa kuwa na mwingine, mahali fulani."

Akasema, "Ninaye mmoja, lakini ninamchukia," akasema, "daima ananikemea."

"Loo," akasema, "mfalme asiseme hivyo, nenda kamlete."

Anasema, "Huyo ni Mikaya, mwana wa Imla."

155 Kwa hiyo mnajua nini? Halmashauri ya mashemasi ilienda kule ikakutana naye, kasema, "Sasa, angalia hapa, Mikaya, kama unataka kurudi kwenye dhehebu tena, yote uliyosema dhidi ya, utasamehewa, kama utasema tu jambo lile lile wanalosema, useme jambo lile lile."

156 Mikaya, ninampenda mtu huyo wa Mungu, akasema, "Nitasema *tu* yale Mungu atakayoweka kinywani mwangu." Kwa hiyo akasimama mbele yake, naye akasema, "Nipe usiku wa leo." Naye hapana shaka aliomba usiku kucha, yapata mapambazuko akaona ono lake. Alipoona hilo ono, akalilinganisha na Neno.

157 Hiyo ndiyo njia ya kuchunguza kama maono yako ni ya kweli au la. Si namna zote za maono ni sahihi. Lakini kama ni kinyume na Neno, achana na ono hilo, bali kama liko pamoja na Neno, dumu nalo.

158 Kwa hiyo Mikaya akatoa unabii wake, kwamba aliwaona Israeli wametawanyika kama kondoo. Sasa, wahudumu mia nne wamesimama pale, wote, vema, wote hao manabii, watu mashuhuri, kikosi cha kikanisa, lakini Mikaya aling'ang'ania, alikuwa amechunguza ono lake kwa Neno, alijua lilikuwa sahihi. Alijua yale yule nabii halisi, Eliya, alikuwa ametabiri, maovu

dhidi ya Ahabu, naye angeweza kusema mema wakati Neno lilisema maovu?

¹⁵⁹ Unawezaje kubariki kile Mungu amelaani, ama unawezaje kulaani kile Mungu amebariki? Lazima iwe pamoja na Neno. Wakati mwingine inakubidi kusimama peke yako, bali simama hapo. Hiyo ni kweli. Ng'ang'ania, dumu moja kwa moja nalo. Haidhuru mtu mwingine yeyote anasema nini, dumu nalo.

¹⁶⁰ Mikaya alidumu moja kwa moja nalo, na bila shaka, tunaona ya kwamba ilithibitika kwamba alikuwa sahihi. Imani kamwe haikanushi ukweli wa Neno, bali hulishikilia hata lionekane la kijinga jinsi gani; imani hushikilia moja kwa moja kwenye kweli ya Neno.

¹⁶¹ Petro, katika kufunga. . . Loo, jamani! Kwa nini mtu fulani hakunivuta? Sikujua ilikuwa inachelewa hivyo. Samahani, marafiki, afadhali nisimame papa basi. Nitatoa matamshi mengine machache tu hapa, mnaona, kisha niende. Hebu tuibadilisha kwa dakika moja tu. Vema, angalieni. Asanteni.

¹⁶² Kulikuwako na Petro, yule mtume. . . Tutalileta nyumbani kwa muda kidogo tu. Petro, yule mtume, alikuwa na maskini baba mzuri, jina lake lilikuwa Yona. Nami ninaweza tu kuwazia Petro, na Andrea, na Yona, walikuwa wavuvi, nami ninaweza kumwona mzee Yona, mwenye umri wa kama miaka themanini, huko nje huku maskini mikono dhaifu ikiwasaidia kuvuta nyavu hizo ndani. Aliona alikuwa akipoteza nguvu zake, alijua haitakuwa muda mrefu sana pia, atawaacha. Ninaweza kumwona ameketi chini kando ya mtumbwi baada ya kuvua samaki wengi siku hiyo, alikuwa ameomba asubuhi hiyo.

¹⁶³ Akasema, "Wanangu, nikaribieni." Huenda alilisema hivi: "Mnajua, sisi watu tumemtazamia Masihi, nasi tunajua Yeye yuaja. Nimetamani sana kumwona, nilidhani hakika Yeye angekuja katika kizazi changu, lakini inaonekana kana kwamba nitaondoka kabla hajaja, ninazeeka. Lakini wanangu, msisumbuke sasa, kabla tu ya kuonekana Kwake kutakuwako na kila namna ya ulokole utakaolizunguka."

¹⁶⁴ Daima ndivyo ilivyo, ni ibilisi, akijaribu kuweka kitishio, mnaona, kuwatishia. Lakini kumbukeni, vitishio daima viko kwenye ule mti mzuri. Kumbukeni tu hilo, si huko nje kwenye supu ya matofaa yaliyochachuka, la, sikuzote viko mahali ulipo mlo mzuri.

¹⁶⁵ Kwa hiyo akasema, "Kumbukeni tu, sasa, kutakuwako na wengine watakaoinuka na kusema wao ni *hivi*, na wengine wanasema wao ni *vile*, na wengine wanasema wao ni *kadhalika*, na kudai Masihi na kadhalika." Kasema, "Kamwe msiamini. Sasa, njia pekee ya kuwa na hakika ni kuchukua yale Neno lisemayo.

¹⁶⁶ "Sasa, Neno lilisema Musa, nabii wa Mungu," nalo Neno daima humjia nabii, yeye alisema, "sasa, Musa alisema

ya kwamba 'Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii kama nilivyo mimi.' Sasa, imekuwa mamia ya miaka tangu tulipomwona nabii. Lakini kumbukeni, Masihi ajapo, Yeye hatakuwa akisema Yeye ndiye *Huyo*. Lakini atakapokuja, Yeye atakuwa ni nabii, nanyi mnamwona. Sasa, Biblia yetu inatwambia kama mtu akidai kuwa nabii, na yale asemayo yanatimia, basi msikieni, kwa sababu mnaweza kumwogopa kwa sababu ametoka kwa Mungu. Lakini, yale asemayo yasiptomia, msiyasikilize, endeeleni tu, mnaona, maana si sahihi. Kwa hiyo sasa ninyi wavulana kumbukeni hilo."

¹⁶⁷ Naye Andrea, mwajua, alikuwa ndiye wa kwanza kumwona, akasema, "Aisee, Simoni, njoo, shuka uende mkutanoni asubuhi, atakuwa hapa chini, makanisa hayatamkubali, kwa hiyo yuko hapa chini mahali pengine. Kwa hiyo wewe shuka uje hapa nami. . ."

"Loo," Simoni akasema, "sasa kumbuka, sisi ni Mafarisayo, nasi—nasi hatuna budi kukaa. . ."

"Lakini na—nataka tu uje, uketi tu chini usikilize kwa dakika chache, uangalie."

¹⁶⁸ Kwa hiyo kesho yake asubuhi, ninaweza kuona baada ya kumaliza kuvuta nyavu, mbona, Yesu akashuka akaja pwani, na—na muda si muda mwajua, hapana shaka Simoni alikuja kwenye kusanyiko, ndipo alipokuja akitembea pale, Yesu aliangalia pale, na kusema, "Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona."

¹⁶⁹ Sasa, nena kuhusu mvulana mwenye kung'ang'ania, alikuwa hivyo tangu wakati huo na kuendelea. Hakuna mtu angaliweza kumfanya atilie shaka wakati huo, alijua. Kwa sababu gani? Alikuwa ameiona ishara hiyo ya Masihi, aliona Neno. Alijua ya kwamba Mtu huyo hakumjua, hakujua jina lake, hakujua lolote kumhusu, na hapa Yeye alimwambia, si yeye tu, bali baba yake alikuwa ni nani, na jina lake lilikuwa ni nani, yule hasa aliyemwambia kuitazamia ile ishara. Aling'ang'ania.

¹⁷⁰ Maskini Filipino, aliposikia hadithi hii, haikumbidi kuona, aliamini, bila shaka alikuwa akimtazamia Masihi. Aling'ang'ania sana hata akazunguka ubavuni mwa kilima, yapata maili kumi na tano, naye akamwona jamaa fulani jina lake Nathanaeli. Haikumbidi kurudi nyuma na kusema, "Sasa, ngoja, hebu na tuketi chini na kuhesabu hili." Akasema, "Njoni, mwone Yule tuliyemwona, Yule ambaye Musa alinena habari Zake." Amina. Ninaweza kumsikia akisimulia hadithi ya Simoni.

Loo, Filipino hu- . . . , ama, huenda Nathanaeli alisema, "Sasa, ngoja kidogo, Filipino, umeingia wazimu."

"Njoo tu, uone. Angalia kama nimeingia wazimu."

¹⁷¹ Kwa hiyo wakati alipoenda kwenye mstari wa maombi, ama katika kusanyiko, popote pale, ninaweza kumwona Nathanaeli akianza kuangalia kote, akisema, “Kwa namna fulani kuna hisia nzuri hapa, usiku wa leo, kwa namna fulani. Inaonekana ni nzuri sana.”

Ndipo akamwona Yesu na Yeye akasema, “Tazama huyo hapo Mwisraeli kwelikweli, ambaye hamna hila ndani yake!” Hilo likamwondolea mawazo mapotovu.

Akasema, “Rabi, ulinijua lini?”

Akasema, “Kabla Filipino hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.”

¹⁷² Ndipo akaangalia kote, akaona wachungaji wake wote, na mashemasi, na wazee wa jimbo, na maaskofu, na wote hao wamesimama karibu, lakini ndugu, aling’ang’ania sana papo hapo, akasema, “Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu.”

¹⁷³ Haleluya! Haya basi. Alishikilia. Kwa nini? Aliona kitu fulani, alisikia kitu fulani, akatambua kwamba kilikuwa ni cha Kimaandiko, kwa hiyo angeweza kusimama aking’ang’ania, haidhuru hao wengine waliwazia nini. Aliona kitu fulani, alikuwa ameshikilia kitu fulani, akakishikilia.

¹⁷⁴ Maskini yule mwanamke kisimani, mwenye sifa mbaya, alikuwa ameona ubandia mwingi sana miongoni mwa watu waliokiri, siku moja yeye... Yapata, hapana shaka ilikuwa yapata saa tano, wakaingia Sikari kununua chakula, hao wanafunzi, huku Yesu, ameachwa peke yake. Baba alikuwa amemtuma huko juu kwa sababu alikuwa na haja ya kupitia huko. Alikuwa akienda Yeriko, lakini alipanda kuuzunguka mlima hadi... maana alikuwa na haja: mtu mmoja, naye ni kahaba. Loo, neema ya ajabu! Mtu mmoja kutoka kwenye kitu hicho chote, naye ni mwenye *sifa mbaya*, akivunja safari Yake ya kawaida mpaka hapa juu.

¹⁷⁵ Yeye, huenda ilikuwa yapata saa tano, alikuja kuchota maji. Huenda alikuwa ameanza kushusha ndoo, mawimbi yake ya nywele yakaanguka juu ya uso wake, naye akaanza kushusha ndoo, akamsikia Mtu fulani akisema, “Nipe maji ninywe.” Akaangalia kote upesi, na huyo hapo Myahudi ameketi.

Akasema, “Si kawaida kwa kitu kama hicho, Myahudi kumwomba Msamaria chochote.”

¹⁷⁶ Kasema, “Lakini kama ungejua ni Nani uliyekuwa unasema naye, ungeniomba Mimi maji unywe.” Alikuwa akifanya nini? Kuwasiliana na roho yake. Baba alikuwa amemtuma huko juu, sasa mhusika yuko huko. Haleluya! Nikaona kitu fulani basi. Ee Mungu! Baba alimtuma huko juu, na sasa huyu hapa huyo mhusika mbele Zake, Hajui la kusema, bali Yeye anaendeleza mazungumzo. Akasema, wakazungumza juu ya ibada huko Yerusalemu, na Wayahudi na kadhalika, na kisima

walichozungumzia, baada ya kitambo kidogo akaona shida yake ilipokuwa, kasema, “Nenda, kamwite mumeo, mje naye hapa.”

Akasema, “Si—si—sina mume.”

Kasema, “Hiyo ni kweli. Umekuwa na watano, na yule uliye naye sasa siye mume wako.”

¹⁷⁷ Akasema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe ni nabii. Tunajua ya kwamba Masihi, aitwaye Kristo, Yeye yuaja, Mtiwa Mafuta, na atakapokuja, atakuwa ni nabii, atatuambia mambo hayo.”

Akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.” Nena kuhusu kung'ang'ania!

¹⁷⁸ Mwajua, kwa kweli haikuwa...kama mnajua desturi ya kimashariki, mwanamke wa aina hiyo hapaswi, kamwe, kumkaribia mwanamume sokoni. Hiyo ni kweli. Si hata wa leo huko India, na mahali mbalimbali. La, bwana. Wanaume hata wasingemsikiliza, kumwangalia, ametiwa alama kama kahaba, wangempa kisogo, haidhuru yeye alisema nini.

¹⁷⁹ Lakini nini? Wasingeweza kumpuuza, wasingeweza kumpuuza mwanamke huyo. Kwa nini? Alikuwa ameshikilia imani. Alikuwa na ujumbe, wasingeweza kumzuia, akasema, “Njoni, mwone Mtu ambaye ameniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi? Je, huyu siye?” Nayu Biblia ilisema mji mzima uliamini kwa sababu ya ushuhuda wa huyo mwanamke.

¹⁸⁰ Maskini yule mwanamke aliyekuwa akitokwa na damu, aling'ang'ania. Ninawazia aliona ma—madhehebu yote yamesimama pale, naye akasonga mbele moja kwa moja karibu nao. Mmoja akasema, “Ngoja kidogo, unaenda wapi? Hivi wewe si mke wa John Doe, huko juu kilimani, ambaye ndio kwanza alibadili lile kundi la farasi, hivi majuzi, kumlipa daktari?”

“Naam, lakini asingeweza kunisaidia kwa vyovyote.”

¹⁸¹ “Vema, wewe ni dhaifu sana, utakanyagwa huko chini, katika kundi hilo la watu. Wasikilizeni, wao si kitu ila kundi la walokole ambao ni takataka za Kigalilaya. Hata hawana dhehebu. Yote afanyayo ni kuyararua makanisa yetu. Rudi huko juu. Nitamwita mchungaji wenu.” Alilipuuza tu, aking'ang'ania, akaendelea kutembea. “Vema, wewe ni dhaifu sana huwezi kwenda mkutanoni.” Hilo halikumkomesha hata kidogo, alikuwa anaenda kwa vyovyote vile, maskini mashavu yaliyoparara, anaenda haidhuru, anaenda kwa vyovyote vile.

¹⁸² Labda mumewe alisema, “Rudi kule juu kilimani, mahali pako.” Mnaona?

“Wewe ni mume wangu, nami nakupenda, lakini sina budi kumgusa Yeye,” akaenda moja kwa moja akampita.

183 Hapa alisimama nani. . . kasema, “Vema, siku- . . .” naye akapita mstari mwingine wa watu. Wakasema, “Siku za miu- . . .” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . ndipo askofu akaja namna *hii*, akasema, “Aisee, tulisikia ulifanya miujiza. Sasa, hebu tukuone ukifanya mwingine.” Mwingine akaingia upande *huu*, upande *ule*.

184 Hatimaye, akawaza, “Nitafanyaje jambo hilo?” Lakini unajua, imani daima hupata njia ya kufanya hivyo, kama yule mwanamke Msirofoinike, imani hupata njia ya kumgusa Yeye. Kama huliamini, anza kuomba sasa hivi, uone kama imani yako haipati njia ya kumgusa; imani hupata njia. Na baada ya kitambo kidogo . . .

Inanikumbusha juu ya—juu ya Abraham Lincoln, wakamfungia nje, mtu mashuhuri.

Wakasema, “Utaingiaje?”

Akasema, “Ni—nitamtumainia Mungu.”

Kasema, “Watakufungia milango machoni pako.”

Akasema, “Bado nitamtumainia Mungu.”

185 Basi maseneta wote walipojibu, walikuwa wakitaka kumtupa nje juu ya mswada huu ambao walikuwa wakijaribu kupiga kura dhidi yake, na kwa hiyo, walijua Abraham Lincoln alikuwa anauunga mkono. Naye alikuwa na presha nyingi sana, na ha—hadhi kubwa sana mbele za watu hata angeweza kuipitisha hoja yake, nao wasingemrusu kuingia mlangoni.

186 Basi waliposimama na kuanza kuyataja majina, waliwaita watu mbalimbali na wengine mbalimbali, na hapo kiti cha Lincoln kilikuwa kitupu, kasema, “Abraham Lincoln?”

Brrruu, huyo akashuka chini kupitia kwenye dohani, kasema, “Nipo!”

187 Imani hupata njia, huenda ikawa ni kushuka kupitia dohani, bali itafika kule. Inaleta tofauti gani, maadamu inafika? Imani hupata njia, huenda ikawa ni kutambaa, huenda ikawa ni kuimba, huenda ikawa ni kupaza sauti, chochote kile, inapata njia yake, inaendelea moja kwa moja.

188 Angejaribu kugusa, huku anafungiwa na kuzuuliwa, hatimaye, akainama tu chini, na kunyoosha mkono, na kugusa vazi Lake, Yesu akageuka, akasema, “Ni nani aliyenigusa?” Kwa nini? Alikuwa na subira, akamgusa.

189 Lazima nifunge, ninajisikia vizuri sana, nachukia kufanya hivyo, lakini tuna mstari mkubwa zaidi wa maombi unaokuja.

190 Sikilizeni, nilikuwa huko Meksiko yapata miaka minne iliyopita, nao walitwambia tungeweza kupata uwanja wa michezo ya fahali. Jenerali Medina alikuwa amenileta huko chini, Mmarekani wa kwanza asiye Mkatoliki aliyewahi kuletwa huko chini.

¹⁹¹ Wakati askofu wa kanisa Katoliki alipomwendea rais, na kusema, “Mheshimiwa, Bwana, mtu huyu anakuja hapa asiye Mkatoliki,” kisha kasema, “amepata msaada wa serikali, kutoka kwa Jenerali Medina, msaada wa kijeshi.” Kasema, “Taifa letu halikubaliani na jambo hilo.”

Na kwa hiyo rais akajibu, akasema, “Mtu huyo ni mtu mwenye sifa nzuri.”

Kasema, “Loo, yeye ni—yeye ni haini tu.”

Kasema, “Sidhani makumi ya maelfu ya watu, wanatoka kwenda kumsikiliza haini.”

¹⁹² Naye akasema—akasema, “Lakini unaona, Bwana,” askofu akamwambia rais, “unaona, Bwana, maskini na wasio na elimu ndio tu wanaoenda kumsikiliza.”

Akasema, “Mmekuwa nao kwa miaka mia tano, kwa nini wao ni maskini na wasio na elimu?” Hilo lilikuwa swali zuri.

¹⁹³ Hawangeturuhusu kuchukua uwanja huo wa michezo ya fahali, kwa hiyo tukapata mahali pakubwa mno huko nje. Ndipo maskini hao Wameksiko... Ninawazia, tunaketi hapa ndani tukisikiliza kwa saa moja na nusu kisha tunachoka, mara nyingi. Hao watu walikuja huko saa mbili ama saa tatu asubuhi, hawana viti, wakasimama, wakiegemeana, siku nzima, nisingekuwa mimbarani mpaka yapata saa mbili ama saa tatu usiku huo, bali walisimama pale kusudi wapate mahali pa kusimama, yapata watu elfu thelathini. Nao hao hapo, wote wameegemeana.

¹⁹⁴ Nilikuwa tu niwe huko siku tatu usiku, nami ninakumbuka usiku mmoja huko, usiku wa pili, akija kupitia jukwaani, nilimwona amesimama jukwaani, Billy alikuwa amemwongoza huko juu, mzee wa Kimeksiko. Miguu yake ilikuwa imejaa sugu, na suruali yake imechakaa kabisa, hana shati, amejifunika tu koti, limechakaa, na kofia kuukuu iliyofungwa kwa kamba. Alikuwa kipofu, huku anaendelea kusema jambo fulani, alipofika karibu nami, alitoa shanga ndogo na kuanza kukariri “Salamu, Mariamu.” Nilimfanya aziache.

¹⁹⁵ Kwa hiyo nikamkumbatia, nikaangalia, ningem-... huku nimevaa jozi nzuri ya viatu, suti,. Yuna haki ya kuwa na jozi ya viatu pamoja na suti kadiri nilivyo nayo. Naam, bwana. Kwa hiyo nikawazia, “Ni—nitampa huyo mzee.” Mnaona? Miguu yake ilikuwa mikubwa zaidi kuliko yangu, mabega yake mapana zaidi namna *hiyo*. Nikaangalia nywele zake zenye mvi, kipofu, nikawazia, “Baba yangu angaliishi, angekuwa na umri kama huo. Na labda yeye ni baba wa mtu fulani.”

¹⁹⁶ Nikamkumbatia, nikaanza kuomba. Ndipo nilipofungua macho yangu namna *hii*, hawafasiri maombi, nilimwona mzee huyo akizunguka huku na huku akiangalia vizuri alivyoweza, mwajua, angeweza kuona na kadhalika, katika ono. Nikatulia

tu kabisa, mara nikamsikia akisema kwa sauti kuu, “Gloria a Dios!” Inamaanisha “Utukufu kwa Mungu.” Angeweza kuona vizuri kama nilivyoweza. Loo, akashuka kupitia pale akaenda *mkuku, mkuku*, upesi alivyoweza. Neema ya ajabu!

¹⁹⁷ Kesho yake usiku kulikuwa na lundo refu kuliko jukwaa hili, limelundikwa juu *hivi*, la shali kuukuu na makoti yaliyowekwa hapo ili kuombewa. Basi nilipofika jukwaani usiku huo, mvua ilikuwa ikinyesha tangu saa nne, asubuhi, watu hao walisimama moja kwa moja kwenye hiyo mvua, hao wanawake wa Kimeksiko huku nywele zao zimefunika uso wao na kulowa maji tu.

¹⁹⁸ Nami ilinibidi kupanda ngazi na kushukia ukutani. Walinichukua kutoka kwenye gari, wakanishusha kwa kamba hizi kwenye ngazi, kufika jukwaani moja kwa moja kando ya ukuta, ambapo nilikuwa nimezunguka huo ukuta kwa gari.

¹⁹⁹ Nami nilikuwa nikizungumza, ndipo Billy akanijia, akasema, “Baba...” Mwanamume wa Kimeksiko, sijui jina lake lilikuwa ni nani, nilimwita “Mañana,” ambalo linamaanisha “kesho,” alikuwa mwenda pole sana. Na kwa hiyo sikuzote alikuwa... Angekuja kunichukua, naye alikuwa karibu... Walimleta kwa sababu asingeweza kuzungumza nami, hakuna mtu anayezungumza nami tunapokuja mkutanoni, naye asingeweza kuzungumza Kiingereza, kwa hiyo nikamwita tu “Mañana.” Na kwa hiyo angepayuka kitu fulani, nami sikusikiliza kamwe maana, sikujua alichokuwa akisema.

²⁰⁰ Kwa hiyo akanikuta jukwaani usiku huo, nami nilikuwa nikizungumza, ndiposa Billy akaja mbio, akasema, “Baba, Mañana alisambaza hizo kadi zote za maombi, na,” kasema, “kuna maskini mwanamke mmoja kule chini, ana mtoto aliyekufa.” Kisha kasema, “Nina zaidi ya mia moja na hamsini,” ama mia mbili, ninasahau ilikuwa ni nini, “mabawabu nao hawawezi kumzuia mwanamke huyo.”

²⁰¹ Kasema, “Ana mtoto huyo aliyekufa pajani mwake, naye atakimbia kupitia katikati ya miguu yao na kukimbia juu ya mabega yao, na kadhalika akiwa na mtoto huyo aliyekufa.” Kisha kasema, “Yeye hapati kadi yoyote ya maombi,” kisha kasema, “tayari tumezisambaza zote. Na kama nikimweka mstarini mbele ya hao watu waliokuja na kuchukua kadi ya maombi, kutakuwa na ghasia kwelikweli.”

²⁰² Na sasa, Ndugu Jack Moore, kuna mtu yeyote aliyepata kumjua Ndugu Jack Moore? Wengi wenu. Alikuwa pamoja nami, kwa hiyo nikasema, “Ndugu Jack, yeye hawezi kututofautisha mimi na wewe,” nikasema, “nenda kule ukamwombe mtoto huyo mchanga, na ita—itakuwa sawa.”

²⁰³ Nao hawa mabawabu wangemshika na kumzuia, naye angesimama pale, mara tu wangegeuza kichwa chao, angekimbia moja kwa moja kupitia katikati ya miguu yao namna *hiyo*, upesi alivyoweza, naye angewavuruga wanne ama

watano wao, nao wangemsukuma nyuma tena, wasingeweza kumwondosha jukwaani. Loo, kung'ang'ania, jamani!

²⁰⁴ Na kwa hiyo, Ndugu Jack akaanza kwenda kumwombea maskini mtoto huyo mchanga, Billy alikuwa akimpeleka kule. Nami nikasema, “Kama nilivyokuwa nikisema,” halafu Ndugu Espinoza, ndugu Mpentekoste kutoka California, alikuwa akitafsiri, nikasema, “sasa, imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.”

²⁰⁵ Ndipo Ndugu Espinoza alipoanza kusema hivyo, niliangalia moja kwa moja hapa nje, yapata futi mbili ama tatu kutoka *hapa*, na palikuwako na maskini mtoto mchanga wa Kimeksiko katika ono, maskini mtoto mchanga, hana meno, ni fizi tu, akinicheka tu. Ndipo nikasugua macho yangu, nikaangalia tena, huyo hapo, maskini jamaa mdogo, alikuwa tu akicheka, hayo macho madogo meusi yamekodolewa tu.

²⁰⁶ Nikawaza, “Sijui kama huyo ndiye mtoto yule.” Nikasema, “Hebu kidogo, Ndugu Espinoza,” naye Ndugu Jack alikuwa akiondoka jukwaani, nikasema, “Waambie hao mabawabu, Ndugu Espinoza, wafanye njia wamwache mama huyo aje huku juu.”

²⁰⁷ Alikuwa amesimama yapata umbali wa jengo hili huko nje, angali anajipenyeza apate njia pamoja na mtoto huyu aliyekufa katika blanketi. Alikufa asubuhi hiyo yapata saa tatu. Daktari alitangaza kwamba amekufa, akafa kwa nimonia. Kwa hiyo yeye. . . Wakafanya njia, naye huyu hapa anakuja, jukwaani, akaanguka chini na kuanza kupaza sauti, “Padre,” maana yake “baba.” Nikajaribu kumfanya asimame.

Aliposimama, Ndugu Espinoza akasema, “Je, ana kadi ya maombi?”

²⁰⁸ Nikasema, “La. Lakini Ndugu Espinoza, usiseme hili, sijui, nimemwona mtoto mchanga wa Kimeksiko katika ono moja kwa moja mbele yangu hapa.” Nami nikasema, “Huenda ikawa ni mtoto wake, nitamwombea tu na kumwacha aondoke namna hiyo.”

Akasema, “Vema.”

²⁰⁹ Nikasema, “Usiyafasiri haya maombi.” Ndipo ni—nikamwambia asimame, naye Espinoza akamwambia katika—katika—katika Kihispaniola asimame, akasimama. Nikasema, “Mtoto wako alikufa lini?”

“Saa tatu asubuhi ya leo.” Ilikuwa yapata saa nne na nusu wakati huo, usiku huo.

²¹⁰ Nami nikasema, “Unaamini?” Kwa moyo wake wote. Hakukuwako na shaka katika nia ya maskini mama huyo, maskini mwanamke mrembo, alionekana yuko kwenye miaka ishirini ya mwanzoni, ishirini na miwili ama ishirini na mitatu, maskini msichana wa Kimeksiko.

211 Kwa hiyo alikuwa na mtoto huyu mchanga na blanketi ndogo juu yake, hiyo hapo ilikuwa imewekwa hapo imelowa maji kabisa, blanketi hiyo, alikuwa amesimama huko nje tangu asubuhi hiyo. Alikuwa ameona makala gazetini kuhusu mzee huyo kufunguliwa macho yake, kwa hiyo alikuwa tayari kumleta mtoto huyo. Na kwa hiyo, nikamwuliza kama aliamini, akasema, “Ndiyo.”

212 Kwa hiyo nikaweka mikono yangu juu ya maskini mtoto huyo mchanga, nikasema, “Baba wa Mbinguni, sasa, sijui, niliona tu ono, na juu ya msingi wa ono hilo, huenda ikawa ndiye huyo mtoto mchanga, hayo tu ndiyo uliyoniambia, nitaweka tu mikono yangu juu yake, nimkabidhi Kwako.”

213 Ndipo maskini mtoto huyo mchanga akafanya, “Whaah,” akaanza kurusha teke kwa miguu yake midogo namna *hiyo*. Ndipo nikaangalia kote, upesi akamwondolea blanketi, nao watu wakaanza kupiga mayowe, nami nikasema, “Sasa, usi—usiseme lolote kuhusu hili, Ndugu Espinoza. Mtafute mkimbiaji, mtafute mtu fulani akifuatilie kisa hicho, nanyi mwende mkachukue taarifa iliyotiwa sahihi kutoka kwa daktari kabla hamjasema lolote,” maana kama utasema lolote kulihusu, halina budi kuwa ni la kweli.

214 Kwa hiyo yeye... Naye akampata mkimbiaji, ndipo kesho yake yeye, mwenyewe, wakamwendea daktari, akatia sahihi taarifa kwamba mtoto huyo alikufa asubuhi hiyo saa tatu. Na hiyo ilikuwa ni usiku huo saa nne, naye huyo mtoto mchanga, nijuavyo mimi, anaishi Meksiko usiku wa leo, mwenye furaha. Kwa nini? Kwa sababu mwanamke, kama maskini mwanamke huyu Msirofoinike, aling’ang’ania. Alijua, alikuwa amemshikilia Mungu, awe Mkatoliki, asiwe Mkatoliki; awe kasisi, asiwe kasisi; awe wa kanisa, asiwe wa kanisa; atengwe, asitengwe; achekwe, asichekwe. Alikuwa nini? Aling’ang’ania, alijua ya kwamba kuna Mungu.

215 Sikilizeni, ishara zilizoahidiwa za Biblia zinathibitisha Yeye hulitimiza Neno Lake. Ishara zilizoahidiwa za Biblia, tunaweza kuzisoma na kung’ang’ania, na kujua ya kwamba Yeye hutimiza Neno Lake.

216 Na tuombe. Kabla hatujaomba, kuna wengine hapa ndani, usiku wa leo, ambao wangetaka kukumbukwa katika maombi haya? Chochote unachohitaji, naomba uinue tu mkono wako, useme, “Mungu, nifanye kung’ang’ania, Bwana, mpaka niweze kupata shauku ya moyo wangu, ni kwa ajili ya utukufu Wako. Bwana, kaa moja kwa moja pamoja nami, jalia nikae pamoja Nawe, nipe kukushikilia Wewe usiku wa leo. Nitaangalia, nitasikiliza, nitaamini. Wakati wengine wanapooombewa, nitaamini, usiku wa leo, nami nitang’ang’ania hata kamwe sitaondoka kwenye jengo hili mpaka nitakapopata nanga katika imani yangu, imani yangu imetiwa nanga ndani yangu,

hasa, hata nitang'ang'ania sana, maana ninaamini. Ninataka kulishika Neno Lako, sasa hivi, kwa ajili ya ugonjwa wangu”?

217 Baba yetu wa Mbinguni, unaiona hiyo mikono. Hadithi ya maskini mwanamke huyu Mmataifa, jinsi ambavyo alishikilia, aling'ang'ania sana, kwa sababu imani ilikuwa imekuja kwa kusikia, na kusikia Neno la Mungu, na pamoja na vizuizi vyake vyote, nasi hapa tumeketi, usiku wa leo, bila theluthi moja ya vizuizi alivyokuwa navyo: Binti yake alikuwa na kifafa, naye alikuwa Mmataifa, ambao Mungu hakuwa ameahidi kuwazuru, alikataliwa na marafiki zake, alikataliwa, labda, na wote tulionena habari zao usiku wa leo, bali tunajua ya kwamba hata Yesu aliijaribu imani yake, akamwambia ya kwamba Yeye hakutumwa kwake, na akasema ya kwamba yeye na jamii yake walikuwa mbwa.

218 Nayo kweli ilikuwa, Bwana, imani inapolishika Neno, inaikubali kweli. Kasema, “Lakini mbwa wanapata makombo.” Ndipo hilo likaugusa moyo wa Bwana wetu, akasema, “Ee mwanamke, imani yako ni kubwa; na iwe kwako kama ulivyoamini.” Basi alipofika nyumbani, kifafa kilikuwa kimemwacha binti yake, naye alikuwa amelala kitandani, ibilisi alikuwa amemwacha.

219 Baba wa Mbinguni, tupe imani hiyo, usiku wa leo. Jalia tuje, na baada ya usiku wa leo tung'ang'anie katika imani yetu, kwa sababu tunaweza kuwa na imani kama tunajua Wewe umeiahidi katika Neno Lako, chochote ulichoahidi, na imani yetu ikishikilie, ni mali yetu. Ulimwambia Yoshua, “Kila mahali nyayo za miguu yenu zinapokanyaga, hapo nimewapa ninyi.” Nasi tunatambua ya kwamba nyayo za miguu zilimaanisha umilikaji.

220 Na Baba, kama baadhi yao, usiku wa leo, hawajawahi kupanda juu vya kutosha kuingia katika Ufalme wa Mungu kumpokea Roho Mtakatifu, jalia wampokee usiku wa leo, jalia wafanye nyayo usiku wa leo, alama za miguu.

221 Halafu hao ambao hawajawahi kufika juu vya kutosha, na kupanda kule juu, na kumiliki baraka ya uponyaji wa Kiungu, jalia waje usiku wa leo, wang'ang'anie, jalia imani iwashike sasa hivi kwa matamshi haya kutoka kwa hawa wengine.

222 Wale ambao hawajawahi kukukubali Wewe kama Mwokozi, jalia wanyoshe mkono usiku wa leo, na wakushikilie Wewe, na kukukubali. Biblia ilisema, “Wote walioamini walibatizwa.” Tujalie, Baba. Na jalia wabatizwe pia, katika maji, na pia katika Roho Mtakatifu.

Tujalie baraka hizi, na umsaidie maskini mtumishi Wako, mnyenyekevu, ninapohudumu sasa, katika Jina la Mwanao, Yesu. Amina.

223 Sasa, ninaamini ya kwamba Billy Paul, kama yuko humu jengoni, alisema ya kwamba alisambaza kadi za maombi, pia

na—nafikiri alisema hamsini. Hiyo ni kweli? Kadi hamsini za maombi. Nasi tunawataka wasimame. Sasa, msiukimbilie, njoni tu mmoja mmoja.

²²⁴ Ni nani aliye na kadi ya maombi namba moja? Mtu fulani? [Ndugu mmoja anasema “A, moja.”—Mh.] (Ati nini?) [“A, moja.”] A, moja. Vema. A, moja, ni yule muungwana? A, mbili, waweza kuinua mkono wako? Sawa. A, mbili. Niliona mkono wa mtu huyo? A, mbili. Vema, Dada. A, tatu, tatu? Vema, nne, tano, inua mkono wako, hata sikuona nne, nne. Vema, anayefuata mstarini. Tano, inua mkono wako. Kadi ya maombi tano.

²²⁵ Sasa, Billy hushuka kwenye kusanyiko, anapanda hapa juu, anachanganya kadi pamoja, anawapa watu kadi, mtu yeyote anayezitaka, mtu yeyote, huna budi kuwa hapa kuzipata, bila shaka. Sasa, nafikiri kama wakija mapema na kupata kadi ya maombi, wanapaswa kuwa na haki ya kuwa wa kwanza hapa juu, sivyo? Vema. Na sasa, lakini Billy hajui ni nani atakayekuwa wa kwanza mstarini, kwa sababu kadi za maombi zimechanganywa, hilo linamsaidia.

²²⁶ Halafu wakati mwingine, ninaanza vinginevyo, kinyumenyume, juu- . . . mmeona likitendeka hata hivyo, kwa hiyo, mnaona. Hiyo ni kweli. Jana usiku hata hatukuwa na kadi zozote za maombi hata kidogo. Mnaona? Mnaona, hilo silo wazo.

²²⁷ Vema, tano, sita, inua mkono wako, saba, vema. Ninapoita—ninapoita namba yako simama. Saba, nane, tisa, kumi, kumi na moja. Njoo tu hapa uingie mstarini papa hapa. Kumi na mbili.

²²⁸ Sasa, kama huwezi kusimama, baadhi ya ndugu watakuja kukuchukua, kukubeba, utakuja hapa juu, naam, bwana. Vema. Kumi na mbili, niliona kumi na mbili? Kadi ya maombi kumi na mbili. Vema. Kumi na tatu, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano. Iweni mkiangalia kadi zenu sasa. Kumi na tano, kumi na tano, kumi na tano, kumi na sita, kumi na saba, kumi na saba, kumi na nane, kumi na nane, nyuma, kumi na tisa. (Asante, Ndugu Vayle.) Kumi na tisa, ishirini, ishirini na moja, ishirini na moja, sikuipata. Ishirini na moja, ishirini na mbili, ishirini na mbili, kadi ya maombi ishirini na mbili. (Asante.)

²²⁹ Nijulishe, mwajua, maana huenda ikawa ni mtu fulani kiziwi, nao wanakosa mahali pao, mnaona, ama mtu asiyeweza kusimama. Mtu fulani aangalie kadi ya maombi ya mwingine, na halafu . . . Angalia kadi yako ya maombi.

²³⁰ Hiyo ilikuwa ni gani, ishirini na mbili? Ishirini na tatu, ishirini na tatu, ishirini na- . . . Kadi ya maombi ishirini na tatu. Ishirini na nne, ishirini na tano, ishirini na sita. Vema. Ishirini na saba, ishirini na nane, ishirini na nane, ishirini na tisa, ishirini na tisa, ishirini na tisa, thelathini. (Asante.) Thelathini na moja, thelathini na mbili, thelathini na tatu, thelathini na tatu, sikuiona. Thelathini na nne, thelathini na nne, thelathini na tano, thelathini na sita, thelathini na sita, thelathini na saba,

thelathini na saba, sikuipata. Thelathini na saba, thelathini na saba.

²³¹ Mwangalie jirani yako kote, huenda akawa na kadi ya maombi, unaona. Thelathini na saba. Huenda akawa ni kiziwi, huenda akaweza. . . hawezi kuamka, mnaona, amepooza, wala hawezi kusogea. Mnaona? Thelathini na saba. Lazima mtu fulani aliichukua kisha akatoka nje. Kama wakiingia, wawekeni mstarini, wawekwe mahali pao sasa, mabawabu watakuwapo kusaidia.

²³² Thelathini na saba, thelathini na nane, thelathini na tisa, arobaini, arobaini na moja, arobaini na mbili, arobaini na tatu, arobaini na tatu, arobaini na nne, arobaini na tano, arobaini na sita, arobaini na saba, arobaini na saba, hilo ni sawa. Arobaini na nane, arobaini na tisa, hamsini, hamsini, mtu yule kule nyuma.

²³³ Sasa, je, watu wote walio na kadi za maombi wamesimama? Kuna mtu mwingine aliye na kadi ya maombi? Kadi zote za maombi zimesimama kwenye safu? Ninataka kuwa na hakika ya jambo hili sasa. Tuliita mmoja, thelathini na saba, nimeona ndugu kadhaa wakiingia tangu wakati huo, nashangaa tu, Nimeita kadi ya maombi thelathini na saba, wala haikujibiwa. Hiyo ndiyo pekee niliyoiona mimi mwenyewe ambayo haikujibiwa ilikuwa. . . [Ndugu Lee Vayle anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] (Ati nini?) Kadi ya maombi namba tano, hivi ilijibiwa? Ndugu Vayle alisema hakuona kadi ya maombi namba tano. Namba tano, ipo, na thelathini na saba?

²³⁴ Sasa, kama mtatupatia tu dakika moja ama mbili, enyi marafiki. Sasa, tutapata. . . Mtu fulani anaingia tena akiwa na mtoto mchanga. Labda huenda ikawa ni baadhi ya wanawake na ndugu inaowabidi watoke pamoja na watoto wao. Na—na kama wako nje sasa na namba hiyo iingie, wawekeni moja kwa moja mstarini, moja kwa moja mahali pao, waweke mahali pa thelathini na saba na tano, na hiyo inafanya kila kitu kuwa sawa wakati huo basi. Thelathini na saba na tano. Kila mtu sasa awe macho, awe chonjo, awe tayari.

²³⁵ Sasa. . . Asante. Hiyo ndiyo njia, hiyo ni bora zaidi. Asante, Bwana. Mnaisikia hiyo vizuri zaidi sasa? Sababu ya wao kufanya hivi ni kwa sababu chini ya upako sizungumzi kwa sauti kubwa sana.

²³⁶ Sasa, wakati wanapowakusanya pamoja, huenda nikasema hivi: Ninalitaka kutoka moyoni mwako, kama huliamini, usiinue mkono wako, lakini kama unaamini, ninataka uinue mkono wako.

²³⁷ Sasa, tunajua ya kwamba Ukristo umekuwa ukikua katika neema ya Mungu katika miaka yote. Martin Luther alikuwa ndiye mrekebishaji wa kwanza kutoka kwenye wakati wa giza, naye alihubiri kuhesabiwa haki kwa imani. Ni wangapi wanaojua hilo? Ndipo Kanisa lilikuwa kama, katika, kama

piramidi, lilikuwa *hapa* chini, kubwa. Mtu yeyote ambaye hata alikiri kuwa Mkristo, alikuwa na hatari ya kuuawa.

²³⁸ Ndipo akaja Wesley akiwa na Ujumbe wa utakaso, ndipo likawa katika uchache zaidi. Ndipo baada ya Wesley likaja kundi la Kipentekoste, ndipo likainuka *juu*. Na mtu yeyote anajua, si kufundisha mafundisho ya piramidi sasa ama chochote kile, ninatoa tu mfano, lakini jiwe la kichwa kamwe halikuwekwa kwenye ile piramidi. Kwa nini? Lilikataliwa. Mnaona? Kwa hiyo kama jiwe la kichwa lingekuja kwenye piramidi. . .

²³⁹ Kama mtu yeyote amewahi kuwa huko Misri, mawe hayo yameunganishwa vizuri sana hata huwezi kuweka wembe kati yayo. Hapo ndipo penye siri, waliyapandishaje huko juu? Yameumana kikamilifu.

²⁴⁰ Sasa, jiwe la kichwa, itabidi liwe ni mawe yaliyotengenezwa, hapa juu, tayari kwa ajili ya jiwe la kichwa, itabidi lichongwe kikamilifu sana, mpaka, wakati jiwe la kichwa litakapokuja, itabidi liumane nayo kabisa kulikamilisha hilo jengo. Hiyo ni kweli?

²⁴¹ Kwa hiyo Kanisa. . . Sasa, kama lile Jiwe la Kichwa lingalikuja katika wakati wa Luther, angalia jinsi lingekuwa kombo. Angalieni kama lingalikuja katika wakati wa Wesley. Inabidi. . . Litakuja katika wakati Wake uliokusudiwa tangu zamani. Lakini Kanisa litachongoka katika hali hiyo mpaka huduma ya Kanisa itafanana sana, na iwe ni huduma ile ile hasa aliyokuwa nayo Yesu, kuifanya yote ilingane kwa ajili ya Unyakuo. Kama vile, kichwa kinajua zaidi ya miguu. Mnaona? Macho yana manufaa kuliko miguu. Macho ni nabii wa Kanisa, huona kimbele. Mnaona? Na vitu hivi vyote huingia kichwani, sehemu ya kichwa.

²⁴² Sasa, ninataka kuwaulizeni swali. Samahani, ndugu, hii inaweza kuwa ni mbali na njia iliyowekwa, lakini kama nimekosea, kunradhi, ninyi, na ninyi ndugu huko nje. Ninaamini ya kwamba Kanisa itabidi lifikie mahali hapo kwa ajili ya Unyakuo, linyakuliwe pamoja ili kumlaki Bwana hewani. Ninaamini ya kwamba tunaishi katika siku hiyo, ambapo Kanisa hakika litakuwa katika uchache, litakuwa ni kundi dogo.

²⁴³ Mnajua, wakati Yesu alipohubiri, hapakuwapo na asilimia mo—mo—moja ya ninii. . . moja kwa milioni moja ya watu duniani waliopata kumsikia. Angalieni wale waliomsikia Yohana akifanya matayarisho. Mnaona? Wateule ndio wanaosikia, hivyo tu. Hiyo ni kweli. “Hakuna mtu awezaye kuja kwangu, asipovutwa na Baba Yangu kwanza. Na wote alionipa Baba watakuja.” Hiyo ni kweli.

²⁴⁴ Sasa, ninaamini ya kwamba kuna Kanisa linalofikia ukamilifu huo, huduma hiyo ya ukamilifu, ambapo zile ofisi, ambapo mitume, manabii, walimu, wachungaji, wainjilisti kwa ajili ya kulikamilisha Kanisa, hao wachungaji, na walimu, na

kadhhalika, watakuwa pamoja sana na Neno mpaka kitu hicho chote kitafanya kazi moja kwa moja hadi Kuja kwa Bwana. Ninaamini hilo, nami ninaamini tunakaribia wakati huo sasa, ninaamini ndivyo ilivyo.

²⁴⁵ Sasa, tunajua ya kwamba Yesu alisema, na ametufundisha kote katika Maandiko, kwamba kazi alizofanya zingefanywa pia. Sasa, ndugu zangu, natumaini kama hawatakubaliana nami, itakuwa . . . itakuwa ni kwa msingi wa kirafiki.

²⁴⁶ Hivi mlifua Biblia inanena juu ya kule kuonekana kwa Bwana, na pia kule Kuja kwa Bwana, na ni maneno mawili tofauti? Lichunguzeni mwone kama hiyo ni kweli. Kuonekana na kule Kuja ni vitu viwili tofauti. Kule kuonekana kwa Bwana ni sasa, Yeye anaonekana miongoni mwa watu Wake. Tunamwona katika kazi Zake zile zile, kule kuonekana, Roho Wake Mtakatifu, lakini Kuja Kwake kutakuwa katika Utu wa kimwili, kutakuwa, kulinyakua Kanisa.

²⁴⁷ Lakini mnaona, tumepitia kwenye Neno, kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Na sasa Kanisa linaingia katika hali nzuri sana, tayari, linangojea. Ofisi . . . Nazo ofisi za Kanisa zinaingia mahali pake, walimu wanaweka mahali hapo, karama zinajidhihirisha zenyewe.

²⁴⁸ Loo, kuna uigaji mwingi sana, hiyo ni kweli, tunatarajia hilo, lakini kuna halisi pia. Kabla hapajakuwapo na dola ya bandia, hapana budi pawe na ya kweli ipate kufanyizwa kutokana nayo. Hiyo ni kweli. Tuna uigaji huo wote wa kimwili, lakini huo hauondoi kutoka kwa yaliyo halisi. Hu—huifanya tu ile halisi kuangaza.

²⁴⁹ Kwa hiyo Bwana sasa anaonekana miongoni mwa watu Wake, ishara kuu na maajabu, akiwafufua wafu, akiwaponya wagonjwa, na kufanya mambo yale yale aliyofanya, ambayo hayajafanywa kwa miaka elfu mbili. Mnaona, Kanisa linachongoka kupitia hilo, limekuzwa hata liko kwenye wakati ufaao. Lile Jiwe la kichwa linakuja kukutana na Kanisa, na itakuwa, wote wataenda pamoja, na kunyakuliwa, wale waliolala katika zamu ya kwanza, zamu ya pili, zamu ya tatu, na kuendelea hadi zamu ya saba. Kuonekana kwa Bwana, jana usiku nilikugusia, jinsi Yeye angekuja.

²⁵⁰ Sasa, kumbukeni, si huyo mtu, hiyo ni ofisi Kanisani. Si mwalimu-mtu wa ajabu, ni mafundisho ya ajabu ya Roho Mtakatifu ndani ya huyo mtu; si yule mtu wa ajabu mwenye karama ya upambanuzi, Roho Mtakatifu wa ajabu mle ndani akimtumia mtu huyo. Mnaona?

²⁵¹ Daima nilisema kama vile Petro alivyorejea wakati mmoja kwenye Mlima wa Kugeuka Sura: mlima mtakatifu. Sio mlima mtakatifu, ni Mungu Mtakatifu juu ya mlima mtakatifu; si kanisa takatifu, ni Mungu Mtakatifu; si watu watakatifu, bali

Roho Mtakatifu. Mnaona? Ni Roho Mtakatifu katika siku hizi za mwisho.

²⁵² Sasa, wakati yule Malaika wa Bwana alipomjia Ibrahimu, hapo katika wakati kabla ya yale maangamizi, sasa, huyo alikuwa ni Mungu akionekana katika mwili wa mwanadamu. Naye Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu, na kama ilivyokuwa katika siku za Lutu.” Yeye alitoa maadili ya yale waliyokuwa wakifanya katika siku za Nuhu.

²⁵³ Katika siku za Lutu, mwangalie yule Mjumbe kwa Ibrahimu, waangalie wale wajumbe kwa Lutu katika kanisa la kawaida, ninii tu, “Tokeni, tokeni,” huku Ibrahimu akiwatetea. Mwangalieni, yule Malaika, Mungu, Elohimu, akionekana katika mfano wa mwili wa mwanadamu ikionyesha ya kwamba Elohimu katika siku za mwisho ataonekana, si kule Kuja kwa Kristo, bali kuonekana kwa Kristo katika mwili wa kibinadamu katika Kanisa Lake, akifanya ishara Zake zile zile na mambo aliyofanya, wala hajafanya hivyo Kanisani kwa miaka elfu mbili, mnaona, kule kuonekana kwa Bwana.

²⁵⁴ Sasa, je, kadi zote za maombi ziko mstarini? Ni wangapi walio wagonjwa huko nje wala hawana kadi ya maombi? Inueni mikono yenu. Fanyeni hivyo tena. Inueni mikono yenu, wote walio wagonjwa, wote wanaoomba, wanaoamini. Vema.

²⁵⁵ Yule mwanamke aliyegusa upindo wa vazi Lake, pia hakuwa na kadi ya maombi, bali aligusa vazi Lake. Nayu Biblia ilisema ya kwamba Yeye, sasa hivi, ni Kuhani Mkuu (Hiyo ni kweli?), anaishi daima kufanya upatanisho, Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Hiyo ni kweli? Nayu Biblia ilisema katika Waebrania 13:8, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Je, hiyo ni kweli?

²⁵⁶ Vema basi, kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, kama ulimgusa kama yule mwanamke alivyofanya, si kimwili, imani yake ilimgusa, kwa sababu Yeye alisema nguvu zilitoka, kila mtu alikuwa akimgusa kimwili, lakini imani yake ilimgusa, naye akageuka, na kujua kutokwa kwake na damu, na kusema imani yake ilikuwa imemwkoa.

²⁵⁷ Hivi huamini Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule usiku wa leo? Na kama maneno haya ni kweli, Yeye anaonekana katika mwili wa kibinadamu, basi mwache aonekane katika mwili wako, akikupa imani katika Neno Lake lililoahidiwa, Yohana Mtakatifu 14:12, “Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya,” basi nitaninii, kama ofisi hizi ziko Kanisani, basi hebu nijitulize mbele zenu, na sehemu ya William Branham iondoke, na kumwacha Bwana Yesu anene kupitia kwangu, aonekane katika mwili wa kibinadamu, kama anavyoonekana katika mwili wako, kwa hiyo kutakuwako na ushahidi wa wawili, na wawili ni thibitisho katika Neno la Mungu, wawili ni

ushahidi. Halafu uwe na imani ya kungusa, nami niwe na imani, na kupitia sisi wawili athibitike Neno Lake kwamba ni kweli.

²⁵⁸ Sasa, ninyi wagonjwa tena, huko nje, sasa, siwezi kushuka kupitia huo, upambanuzi, kupitia mstari huo, mnajua hilo, lingeniondoa moja kwa moja jukwaani. Maskini mwanamke m—mmoja alimfanya Mwana wa Mungu kusema alikuwa dhaifu, huku Yeye ni Mwana wa Mungu. Mnafikiri ningekuwa je, mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema Yake?

²⁵⁹ Hata nisingeweza kustahimili mmoja wao kama Yeye hakusema, “Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya, na nyingi kuliko hizi mtazifanya.” Ninajua King James inasema “kubwa zaidi” lakini kwa kweli ni “nyingi zaidi.” Mnaona? Ati kubwa zaidi? Asingeweza kufanya kubwa zaidi, aliwafufua wafu, akasimamisha maumbile, akafanya kila kitu. Mnaona? Kwa hiyo ni nyingi tu zaidi yake, kwa sababu kungekuwa na watu wengi zaidi, Roho alikuwa tu katika Mtu mmoja pale, sasa ni kote ulimwenguni, ulimwenguni, katika watu Wake wote.

²⁶⁰ Aminini. Hebu tuchukue tu kwa kuanzia, umati huu kwa njia hii. Ni wangapi hapo wasionijua mimi, nami siwajui ninyi, nawe ni mgonjwa, nawe unaamini ya kwamba Mungu anaweza kukufunulia shida yako? Inueni mikono yenu. Ninyi nyote huko msio na kadi za maombi, nanyi mnataka kitu fulani kutoka kwa Mungu, inua mkono wako; hapa ndani; hapa. Ombeni.

²⁶¹ Hebu nigeuze mgongo wangu. Ninyi ombeni. Malaika aliyeonekana katika mwili wa mwanadamu alikuwa ameelekeza mgongo Wake kwenye hema alimokuwa Sara, Naye akamwambia Sara yale aliyofanya. Hiyo ni kweli? Malaika uyuo huyo alikuwa ni Mungu, na Mungu yeye yule aliyekuwa pale aliahidiwa na Yesu, Yule aliyekuwa ni Mungu, kuonekana katika siku hizi za mwisho kabla ya kuteketezwa kwa dunia, kama tu alivyofanya katika siku za Sodoma. Mnaamini?

²⁶² Bila shaka ni ono, kuna watu wanaosimama hapo nisiowajua, ingekuwa ni juu Yake. Hii hapa. Kama ninaweza kuona mahali ilipokuwa, naam.

²⁶³ Mama aliyeketi papa hapa, mnene, je, uliinua mkono wako dakika chache zilizopita? Unaamini Mungu atakuponya hiyo baridi yabisi na kukupa afya? Kama unaamini, inua mkono wako. Vema. Unaweza kuupata.

Aligusa nini?

²⁶⁴ Mwanamume huyo aliyeketi karibu naye, unaonaje, Ndugu? Unaamini hilo linatoka kwa Mungu? [Ndugu huyo anasema, “Naam, bwana.”—Mh.] Unaamini? Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini? Ungeamini? Je, ungekubali kama ningeweza kukwambia kwa Roho wa Mungu? Ninazungumza hapa, uliyeketi karibu nami. Unaamini? Utaamini? Vema basi, shinikizo lako kuu la damu litakuacha.

²⁶⁵ Mtu huyo aliyeketi karibu nawe alikuwa na jambo lile lile, maskini huyo mtu mwembamba hapo, alikuwa na shinikizo kuu la damu pia. Kama hiyo ni kweli, inueni mikono yenu, nyote wawili. Haleluya! Nendeni mkiamini, msiwe na shaka.

²⁶⁶ Waligusa nini? Hawakunigusa mimi. Siwajui watu hao, sijawahi kuwaona maishani mwangu. Ninyi nyote ni wageni kwangu. Hiyo ni kweli. Mkiamini tu, hilo tu ndilo mnalopaswa kufanya.

²⁶⁷ Huyu hapa maskini mama mmoja ameketi hapo, papo hapo nyuma, akiniangalia moja kwa moja. Anaingia upesi tu katika Ufalme wa Mungu. Anawaombea wanawe ambao hawajaokoka. Kama utaamini kwa moyo wako wote, wataokoka. Utaamini? Vema. Unaweza kuupata.

Mnaamini, ninyi nyote?

²⁶⁸ Unaamini Mungu atakuponya huo wasiwasi, Bwana, unayeketi hapo? Ulikuwa ukimwomba alifanye papo hapo. Vema, yote yamekwisha, unaweza kuupata.

²⁶⁹ Maskini mama aliyeketi hapa nyuma, akimwombea mjukuu huyo, unaamini ya kwamba Mungu atamponya? Amedumaa, lakini unaamini ya kwamba Mungu atamponya? Unaamini kwa moyo wako wote? Unapanga kumleta kanisani kesho usiku, haitakubidi kufanya hivyo. Mungu atamponya, nanyi mnaweza kumleta. Vipi kuhusu hilo, Mama? Unaamini? Vema, unaweza kuupokea.

Mimi ni mgeni kabisa kwa mwanamke huyo. Simjui hata kidogo, sijawahi kumwona maishani mwangu.

Hatufahamiani, Mama? Kama ndivyo, inua mkono wako. Hivi hilo silo ulilokuwa ukiombea? Basi, pungu mkono wako namna *hiyo*.

Hivi hamwoni? Elohimu, Mungu. Mnawezaje kutilia shaka? Hivi hamwezi kung'ania?

²⁷⁰ Ili kuanzisha tu hapa mstarini, sasa, ulikuwa na kadi ya maombi, hawakuwa nayo. Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Unaamini nimewaambia ukweli, usiku wa leo, juu ya Neno la Mungu? Sikujui, sijawahi kukuona maishani mwangu, hatufahamiani nijuavyo mimi. Lakini unaamini kama Mungu unaweza kuniambia shida yako, ama kitu ambacho wewe, uh, kitu ambacho wewe, utajua kama ni kweli ama si kweli. Unajua kile kilicho...Kama ninaweza kukwambia kile kilichokuwako, na kukwambia kile kitakachokuwa, mbona, unajua hilo litakuwa sahihi.

²⁷¹ Huko hapa kwa ajili yako mwenyewe, unasimama kwa ajili ya mtu mwingine, naye mtu huyo hayuko hapa. Huyo ni mke wako, yuko katika jimbo lingine, yuko Georgia, ana tatizo la figo, yeye ni mgonjwa sana, ana matatizo. Hiyo ni kweli, sivyo? Unaamini kwa moyo wako wote sasa? Nenda nyumbani

ukamkute, jinsi ulivyoamini, hivyo ndivyo utakavyomkuta. Amina.

Kamwe usiwe na shaka. “Kama unaweza kuamini, yote yanawezekana kwa hao waaminio.” Amina.

Huyo alikuwa ni mwanamume, huyu hapa mwanamke. Hebu na tuwe na mmoja tu zaidi, na kisha tutaanza tu kuwaombea wagonjwa, tuone kama tunaweza kushuka kwenye mstari huo. Mnaona?

²⁷² Njoo karibu nami, Dada. Ninaamini hatufahamiani. Hatuninii. . . sisi ni watu wawili tu waliokutana hapa, jinsi ile ile, katika mandhari kama hii huko Sikari, ambapo Yesu alikutana na yule mwanamke kisimani, sisi hapa, mwanamume na mwanamke walikutana, mara ya kwanza maishani.

²⁷³ Loo, jamani! Laiti—laiti—laiti ningaliweza kuona nguvu za Shetani zikiondolewa! Tunawezaje kusimama na kuona jambo hili halafu tusiamini?

²⁷⁴ Huyu hapa mwanamume na mwanamke, hatujawahi kuonana. Yeye ni mwanamke tu aliyesimama hapo, sijui hata jambo moja, sijawahi kumwona maishani mwangu. Sasa, vipi kuhusu jambo hilo? Sijui hata jambo moja. Vema, ni kitu gani? Mungu aliahidi jambo hilo, Neno la Mungu linasema hivyo.

²⁷⁵ Aliniahidi hilo usiku mmoja huko juu, na miaka mingi iliyopita alisema nilizaliwa kwa ajili ya jambo hili, ninaliamini. Mara makumi ya maelfu, kote ulimwenguni, na hakuna hata wakati mmoja ambapo limewahi kushindwa. Ni kitu gani? Inakuonyesha ya kwamba wakati umekaribia. Si mimi, ni Yeye. Ningemjuaje mwanamke huyu?

²⁷⁶ Maskini ndugu mdogo ambaye mwanaye aliponywa, alisema, “Ninajua haina budi kuwa ni Mungu, Ndugu Branham, watu katika ujirani wangu, ninaowajua.” Kisha kasema, “Ninajua ni ahadi kwa ajili ya siku hizi za mwisho na iko hapa.”

²⁷⁷ Biblia, katika Malaki 4, iliahidi jambo hilo. Alisema haina budi kutimia kabla haijaja ile siku ya Bwana iliyo kuu na ya kuogofya, itakayoiteketeza dunia. Nasi tunajua tunaishi katika siku hiyo.

²⁷⁸ Hawa hapa watu wawili wamesimama hapa, simjui mwanamke huyo. Nne, tano, sita, saba, ama chochote kile, chochote kile kilichokuwa huko nje, na kuna mstari mzima, laiti ningaliweza tu kusimama hapa muda mrefu kutosha. Hilo ndilo ninalojaribu kufanya sasa, nijitikise vya kutosha hata niweze kuendelea na mstari wa maombi. Anakufanyia jambo fulani, ni kama kitu kinachoendelea kama m—mpwito huko nje kwenye kusanyiko hilo, *tuu, tuu*, ni imani.

²⁷⁹ Loo, laiti ungaliweza tu kuvunja kizuizi hicho kidogo hapo, uwe huru! Kama vile ndege akitoka kwenye kizimba, ana mabawa, atokee tu mlangoni.

280 Mama, kuongea nawe tu kwa dakika moja sasa, sikujui, bali Mungu anakujua. Basi kama itakubidi kusema jambo fulani, kwamba kama... Kama Yeye ataniambia jambo fulani kukuhusu wewe, kile kilichokuleta hapa, kama yule mwanamke alivyoligusa vazi Lake, ama kitu kama hicho, ishara fulani ya Biblia kuonyesha ya kwamba ni... u—unajua haina budi kuwa ni kitu fulani, kwa sababu sikujui. Basi, kama wewe... kama ingekuwa, unajua kama ingekuwa ni kweli au la, maana unajua habari zake. Halafu basi, kama ni kweli, jamani, hilo si lingekuwa zuri sana? Jamani, bila shaka lingekuwa!

281 Sasa, huyu mama ni mgonjwa sana, ninaiona sasa. Ninamwona kwa daktari, yeye, amekataliwa na daktari. Anaugua kila namna, magonjwa ya ziada. Jambo moja, una ngiri, na unapaswa kufanyiwa upasuaji, nawe una moyo mbaya sana hata hakuna daktari atakayeshughulikia ugonjwa huo. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI, lakini kuna Mmoja hapa atakayeushughulikia ugonjwa wako...?.. Usiwe na shaka...?.. Endelea kuamini kwa moyo wako wote.

Unaamini? Amina...?..

282 Sasa, unajua ninajua shida yako, kama nilikwambia au la, kama nikikuombea, unajua kuna namna fulani ya upako hapa. Hiyo ni kweli? Unaamini? Hakika, utaamini.

Baba yetu wa Mbinguni, mponye dada yangu usiku wa leo, na kuufanya ugonjwa huu...?.. katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

“Maombi ya imani yatamwokoa mgonjwa yule, Mungu atamwinua.”

283 Unajua kwamba ninajua shida yako. Ingesaidia kama ningekwambia, ama ungeninii tu... Kama ningekuombea, unajua kuna namna fulani ya upako hapa unaojua una shida ya moyo... Samahani. Endelea, yote yamekwisha...?..

284 Sasa, ulipokuwa umeketi pale nje dakika chache zilizopita, nami nikamwomba mtu yeyote aliyekuwa na haja kuinua mkono wake, uliinua mkono wako. Ndipo ulipoinua mkono wako hisia ya ajabu sana ilikugusa, sivyo? Kwa sababu, hapo ndipo wasiwasi wako ulipokuacha. Nenda zako na...?..

285 Kama ningekuombea, ungepona hata hivyo, sivyo? Lakini ingekusaidia kama nikikwambia kilichokuleta hapa? Ingekusaidia? Shida ya kike, shida ya akina mama. Unaamini sasa? Nenda ukapate afya, kama unaweza tu kuamini kwa moyo wako wote.

Sasa, vipi kama nikiweka tu mikono yangu juu yako, na kukuombea tu, utaniamini?

286 Baba wa Mbinguni, mjalie huyu...?.. Yesu, Wewe ulisema, “Ni kubwa vipi imani yao...thawabu yao wale ambao

hawajapata kuona, lakini wanaamini!” Ninaomba ya kwamba utamponya, Baba, lijalie...?...

Unajua kwamba ninajua tatizo lako. Haikufai kitu, hata hivyo, kama nikikwambia. Unaamini kama nikikuomba tu?

Baba wa Mbinguni, jalia asikohoe tena, jalia kiondoke, jalia aponywe, katika Jina la Yesu.

Unaamini?

Njoo, Ndugu. Kama ningeweza kukuponya, ningekuponya. Siwezi kukuponya, ninaweza kukuomba. Unaamini Yeye atanisikia? Njoo hapa.

Baba yetu wa Mbinguni, ninambariki ndugu yangu katika Jina la Yesu Kristo, Mwanao. Mjalie uponyaji wake. Amina.

Amini, usiwe na shaka, sasa.

Njoo, Bwana. Unaamini atasikia maombi yetu? Kama ningeweza kukuponya, ningefanya hivyo, siwezi, ninaweza tu kuomba. Unaamini?

Baba wa Mbinguni, kama yule mwanamke Msirofoinike, jalia apate shauku yake usiku wa leo, aende nyumbani na awe mzima katika Jina la Yesu. Amina...?...

²⁸⁷ Njoo, Dada. Unaamini nikikuomba, ungepata nafuu? Itakuwa faraja kubwa, sivyo? Wamejaribu kila kitu, maskini Asthimador na kadhalika, bali kamwe hazifai kitu. Lakini Mungu ndiye Mponyaji. Unaamini hiyo ni kweli?

²⁸⁸ Baba yetu wa Mbinguni, ninaomba katika Jina la Yesu ya kwamba utamponya mwanamke huyu, na kumpa afya. Ninaweka mikono yangu juu yake, Bwana. Ninaamini ya kwamba Roho Wako yupo hapa, na ametutia upako. Ninaomba ya kwamba utamponya. Amina.

“Kuomba kwa imani kutamwokoia mgonjwa yule, naye Mungu atamwinua.”

²⁸⁹ Ninyi...Sasa, iweni na kicho kabisa, kaeni kimya. Sasa, mnaona, huenda Yeye akaita kitu fulani huko nje, na kama mnazunguka-zunguka siwezi kulishika, mnaona, maana kila mmoja wenu ni roho, na mle ndani, unawasiliana, unaona, unapofanya hivyo, unapojongea inanivuruga, mnaona. Mnaelewa? Mnaona? Yesu alimchukua mtu na kumwongoza moja kwa moja nje ya mji, mbali na kutokuamini kwote. Mnaona? Ketini kimya kabisa, na mwe katika maombi.

²⁹⁰ Huyu hapa mama mmoja. Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini? Ungekubali hilo? Hebu niangalie. Una uvimbe. Unaamini Mungu anaweza kuniambia uvimbe huo uko wapi? Uko kwenye utumbo. Hiyo ni kweli. Unaamini ya kwamba Mungu atauponya? Basi nenda, kama ulivyoamini, ndivyo itakavyokuwa kwako...?...Vema.

Mungu hana upendeleo, kama alimponya yule mama anayeshuka kule mwenye ugonjwa wa kike, anaweza kukuponya pia. Kwa moyo wako wote.

²⁹¹ U hali gani, Dada? Unaamini kama nikimwomba, Yeye atakuponya? Siwezi—siwezi kukuponya, bali ninaweza kumwomba, kama angeweza kukuponya. Ninaamini tayari umeponywa. Hivi huoni hivyo? Vema. Hiyo ndiyo njia ya kufanya jambo hilo. Mungu akubariki.

Hiyo ndiyo njia, hiyo ndiyo njia.

²⁹² Unaamini kama tutamwomba Mungu . . . ? Yesu alisema hivi: “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa watapata afya.” Unaamini kwamba ninamwamini Yeye? Basi, katika Jina la Yesu Kristo, ninatii amri Yake ya kuwawekea mikono wagonjwa. Amina. Uponywe.

²⁹³ Utaamini pia, Dada? Unaamini, unayepitia hapa? Wewe—wewe huji tu kupitia karibu na Ndugu Branham, maana haingefaa chochote, bali unakuja, ukiamini ya kwamba Kristo amesimama hapa mahali fulani, wala hatumwoni. Hiyo ni kweli? Njoo.

Baba wa Mbinguni, ninambariki mwanamke huyu, katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe. Amina.

Amini sasa.

Unaamini, Dada?

Baba yetu wa Mbinguni, ninaomba kwamba, katika Jina la Yesu, ya kwamba utamponya dada huyu na kumpa afya . . . ? . . . Amina.

Mungu akubariki, ndugu yangu, kipofu jichoni na, loo, jambo baya sana. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya?

²⁹⁴ Baba yetu wa Mbinguni, Wewe pekee ndiye unayeweza kumponya mtu huyu. Ninamwombea, huku mikono yangu ikiwa juu yake, na kuomba ya kwamba ataponywa kabisa. Tujalie, katika Jina la Yesu, ninaomba. Amina.

Mungu akubariki, ndugu yangu, nenda ukiamini.

Wewe amini pia, Dada.

Baba wa Mbinguni, ninaomba kwa ajili ya uponyaji wake katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu awabariki.

²⁹⁵ Njoni moja kwa moja. Ni nyote wawili? [Ndugu huyo anasema, “Naam.”—Mh.] Vema, nawatakia heri. Jamani, hili ni tamu. Natumaini siku moja kumwona baba na mama yangu wakishuka kupitia katika Ufalme wa Mungu. Kama nikiwaombea, mnaamini ya kwamba Yeye atawaponya?

²⁹⁶ Baba yetu wa Mbinguni, maskini hawa mume na mke, ninaweka mikono yangu juu yao kwa uchaji wote na

heshima ni juavyo. Na kama ingekuwa katika uwezo wangu, ningewaponya. Siwezi kufanya hivyo, Bwana, bali ninakuamini Wewe, ambaye utawaponya. Ninaomba hilo, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Nenda sasa, na nyote wawili mpate afya, na mkaishi maisha mazuri, yenye furaha, na marefu kwa ajili ya Ufalme wa Mungu.

²⁹⁷ Hilo ndilo jambo la kuchukiza sana, um-hum, hakuna ajuaye kulihusu. Unaona? Kila mtu anakwambia, “Jirudie,” nawe unawezaje? Huh? Unaona? Wasiwasi. Looo, jamani, maskini kivuli hicho cheusi kinachokufuata wakati wote, hakuna kitu unachoweza kufanya. Kila kitu kimeenda kombo, na kila... Jambo ndilo hilo. Unaamini Yeye ataniruhusu nikiondoshe kwako?

²⁹⁸ Shetani, toka kwake. Katika Jina la Yesu Kristo, achana na maskini mwanamke huyu. Jionee aibu! Ninakuapisha kwa Mungu aliye hai, ambaye Uwepo Wake upo hapa sasa, ambaye mimi ni mtumishi Wake, na iwe tangu usiku huu na kuendelea. Amina.

Mungu akubariki, Mama. Kwa imani yangu yote na tumaini langu, uko huru. Nenda zako ukishangilia, ukisema, “Asante...?...”

Unaamini, ndugu yangu? Na tuombe.

Baba wa Mbinguni, katika Jina la Yesu Kristo, Mwanao, jalia nguvu zilizomfua Yesu kutoka kaburini zihuishe mwili wake na kumpa afya. Amina.

Bwana akubariki, ndugu yangu.

Unaamini, Dada?

²⁹⁹ Baba yetu wa Mbinguni, katika Jina la Yesu, Mwanao, ninaweka mikono yangu juu ya mwanamke huyu wakati tukiwa Mbele za huu, Uwepo wa Yesu Kristo uliofunikwa. Jalia aponywe. Amina.

Ubarikiwe, Dada. Nenda tu ukishangilia, ukifurahi, ukiamini.

Njoo, Dada, wewe na Ndugu; hebu tushike mikono yenu.

³⁰⁰ Baba wa Mbinguni, ninawabariki. Katika Jina la Yesu Kristo na wapate shauku zao usiku wa leo, waponywe kabisa, na kuuishia Ufalme wa Mungu, katika Jina la Yesu. Amina.

Nenda ukiamini sasa. Usitie shaka, amini tu.

³⁰¹ Mnaweza kuamini? Kila mtu anaamini? Mara nyingi watu wanafikiri una... kila mtu hana budi kuambiwa. Haikubidi kuambiwa, najua hilo, na kama nikianza kulizungumzia, basi yanaendelea tu kuwa mengi zaidi, na zaidi, na zaidi, mnaona, nami ninaendelea kudhoofika zaidi, zaidi, zaidi, huku mstari ungali ni mrefu. Lakini Mungu anajua kila kitu. Hivi hamwamini

hilo? Bila shaka, Yeye hufanya hivyo. Ni wangapi wanaoamini, kama ukisema lolote ama husemi, unaamini tu? Amina.

Sasa, Yeye hakuniacha, nilipoanza tu jambo hilo, Yeye angali hapa, Yeye yupo hapa. Mnaamini hilo?

³⁰² Na wewe je? Unaamini? Sikujui, Mungu anakujua. Lakini unaamini Yeye anaweza kujua shida yako? Kama nikikwambia, utashangaa. Unadhoofika sana, una vipindi vya udhaifu. Hiyo ni kweli. Unaamini ya kwamba Yeye anaweza kukuponya kutokana na huo? Mhubiri anayetaka kuihubiri Injili? Wewe ni mhudumu, nawe unaingiwa na udhaifu sana hata huwezi kuhubiri. Hiyo si ni kweli? Lakini unaweza kuwa na nguvu tangu sasa na kuendelea. Unaamini ndivyo ulivyo? Basi nenda zako, useme, “Bwana asifiwe.” Amina. Hebu nisikie kutoka kwako.

Haleluya! Amina.

³⁰³ Loo, Marekani, Marekani, ni mara ngapi Mungu angewakusanya, ni mara ngapi, lakini nyinyi. . . ? . . .

Kitu cha kigeni kukuhusu. Loo, najua sasa, hili hapa: Wewe ndiye yule mama niliyekutana naye mkahawani. Imekwisha.

³⁰⁴ Katika Jina la Yesu Kristo, jalia mwanamke huyu aende nyumbani sasa, akiwa mzima. Bwana, jalia aponywe huu, ninaamini Wewe utafanya hivyo, kwa sababu leo hii ule mwongozo mkuu wa kisiri kwenye mkahawa ule, ukijua ni kitu gani kilichosababisha jambo hili, maskini mwanamke huyu amejaribu kujitikisa kutoka kwake kwa muda mrefu, lakini sasa anawekwa huru.

Nenda katika Jina la Yesu ukapate afya. Nenda kwa furaha, ukishangilia, amini.

Vema, Bwana. Unaamini kama nikimwomba, utaponywa?

Katika Jina la Bwana Yesu Kristo, jalia uponyaji wa ndugu yangu, ninapomwekea mikono, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Amina.

Mungu akubariki, ndugu yangu. Nenda.

Mungu akubariki, ndugu yangu. Siku nyingi zimepita hapa. Na tuombe.

³⁰⁵ Baba yetu wa Mbinguni, loo, laiti ningaliweza kumshika baba yangu usiku wa leo, namna hii, bali ni wake. Msaidie, Mungu, mbariki pia, Baba. Jalia wapate uponyaji, waishi maisha marefu, na siku moja Utukufuni, wakati ambapo sisi sote tumegeuzwa kuwa vijana tena, jalia nikutane nao tena, ushuhuda wa Yesu Kristo; ninaomba baraka hii. Amina.

Mungu awabariki. Nenda zako, ukiamini, uwe mzima. Mwamini tu Mungu. Mungu akubariki.

Hiyo si ni tamu?

³⁰⁶ Unaamini, Kijana Mwanamume? Katika Jina la Yesu Kristo, ninatii amri Zake kwa kuweka mkono wangu juu ya wako, na kumwomba ibilisi akuondokee, nawe upate afya.

Unaamini, Dada?

Basi, katika Jina la Bwana Yesu Kristo, Wewe ulisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio,” jalia apone. Amina.

Usitie shaka, nenda tu sasa, ng'a- . . . ng'ang'ania. Liamini.

U hali gani, Dada? Hii ndiyo saa ya ukombozi kwako. Unaamini?

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia awekwe huru sasa hivi. Amina.

Utaponywa. Mungu akubariki, Dada.

³⁰⁷ Njoo hapa. Ndugu, najua fimbo ya kale inavyomaanisha, kuchehelea nayo. Hii itakuwa ndiyo ile saa ya ukombozi. Je, utang'ang'ania, katika Uwepo wa Mungu sasa, si mbele zetu, bali Uwepo Wake, kwamba nitakuombea, nawe utapata afya? Unaamini hilo?

Baba yetu wa Mbinguni, ninambariki ndugu yetu. Katika Jina la Yesu Kristo, na jalia nguvu za Mungu zimponye. Amina.

Amini sasa, Ndugu. Ninii yako yote . . . ? . . .

Jamaa mdogo.

Jalia maskini jamaa huyo awekwe huru. Katika Jina la Yesu Kristo, na jalia iwe tangu usiku wa leo na kuendelea. Amina.

Sasa, angalia kinachompata. Alikipata.

³⁰⁸ U hali gani, Bwana? Jamani, maskini mkono huu wa kale uliolemaa! Laiti ungaliweza kuunyosha kwa Bwana Yesu usiku wa leo, na kumwacha akubariki na kukupa afya.

³⁰⁹ Baba wa Mbinguni, ninamwombea mvulana huyu, ninaomba ya kwamba zile Nguvu zinazoweza kumfanya mzima, Yesu Kristo, zitamponya. Jalia arudi, akionyesha ya kwamba baraka za Mungu zimekuja juu yake, katika Jina la Yesu Kristo. Asante, Bwana.

Mungu akubariki, Jamani. Nenda ukiamini sasa.

U hali gani, Jamaa Mdogo? [Ndugu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Ninaamini atafanya hivyo, sivyo?

³¹⁰ Mvulana huyu mdogo hawezi kuzungumza. Unaona? Kwa hiyo amini tu. Sasa, tutaomba na kumsihi Mungu. Ninaamini mvulana huyu mdogo atarudi akizungumza. Hakika, atazungumza. Unaamini hili?

Ana bo—bomba mbaya? [Ndugu huyo anasema, “Naam.”—Mh.] Jamani, jamani!

Baba yetu wa Mbinguni, jalia pepo bubu juu ya mtoto huyu aondoke, na jalia huyu mtoto azungumze. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

...?. . . kesho usiku . . . ? . . .

³¹¹ Mungu mwenye rehema, aliyemfufua Yesu kutoka kwa wafu, mponye dada huyu na umpe afya, ninapoweka mikono yangu isiyostahili juu yake, bali nikimwamini Kristo, Yule anayestahili, ninaomba kwa ajili ya uponyaji wake. Amina.

Ubarikiwe, Dada. Amini sasa.

U hali gani, Dada?

³¹² Baba yetu wa Mbinguni, mwanamke huyu anapopita jukwaani kwa unyenyekevu, kwa uchaji, tukijua ya kwamba uponyaji ni jambo ambalo tayari limefanywa. Watu wanaamini, basi, kama nilivyosema usiku wa leo, wawe kama yule mwanamke wa zamani za kale, mwenye kung'ang'ania, mvumilivu, Wanaamini hilo. Mungu anawaonyesha ishara Yake, wanaikubali, wanaiamini. Jalia aponywe, katika Jina la Yesu. Amina.

Unaamini, Dada?

³¹³ Baba yetu wa Mbinguni, "Kuomba kwa imani kutamwoko mgonjwa yule, na Mungu atamwinua," ninaomba ya kwamba utamjalia dada yetu baraka hii, kile aombacho, katika Jina la Yesu Kristo, ninaweka maombi yangu pamoja na yake, imani yangu pamoja na yake, na jalia itimizwe. Amina.

Mungu akubariki, Dada.

³¹⁴ U hali gani, Dada? Unaamini ya kwamba Yeye atakuponya? Nitaweka imani yangu pamoja na yako nasi tutaweka maombi yetu juu ya madhabahu Yake, na kuamini katika Uwepo Wake.

³¹⁵ Baba yetu wa Mbinguni, ninamwombea mwanamke huyu mpendwa anaposimama hapa, usiku wa leo, amelemaa, mambo haya yote, Baba, ninaomba ya kwamba—ya kwamba utamjalia kupona, Mungu. Ninaweka maombi yangu juu ya madhabahu pamoja na yake, nikiweka imani yangu juu ya ile dhabihu, Kristo Yesu, na kuomba ya kwamba atapata afya. Amina.

Amini sasa, kwa moyo wako wote.

U hali gani, Ndugu? Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya?

³¹⁶ Baba yetu wa Mbinguni, wakati huyu kijana mwanamume anayeonekana shujaa anaposimama hapa mbele yangu. Tunasimama katika Uwepo Wako kama ndugu. Ninakuomba Wewe, Bwana, ninapoweka maombi yangu pamoja na yake, mjalie, Bwana, ya kwamba ata—ya kwamba atatimiziwa haja yake. Katika Jina la Yesu. Amina.

Liamini sasa, shikilia, lishikilie, limeombwa, kwa hiyo na lifanyike.

U hali gani, ndugu yangu? Unaamini pamoja nami sasa kwamba unaweza kurudi chini kusini, mzima?

317 Baba yetu wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamjalia haja yake. Ninaweka maombi yangu pamoja na maombi yake, imani yangu pamoja na imani yake, yote katika Biblia yako na katika Damu ya Yesu Kristo, tunaomba, katika Jina Lake. Amina.

“Kuomba kwa imani kutamwoko mgonjwa yule, na Mungu atamwinua.”

Ndugu yangu, utaamini pamoja nami, sivyo?

318 Baba wa Mbinguni, ninapoushika mkono wake, jalia nguvu za Mwenyezi Mungu zije juu ya ndugu yetu, na jalia kila shaka dhaifu inayotaribu kushikilia, iachiliwe. Jalia apite kizuizi hicho cha sauti, aendele, na kuvuma huko nje, katika Ufalme wa Mungu, akishikilia, akidai kuponywa kwake kwa kupigwa kwa Bwana wetu Yesu Kristo. Amina.

Ubarikiwe, Ndugu.

U hali gani, Dada? Ninaamini hii ndiyo saa.

319 Ninaweka imani yangu pamoja na ya dada yangu juu ya madhabahu takatifu ya Mungu pamoja na maombi yangu na imani yangu pamoja na yake. Ninamwomba, Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, ampe, haja yake. Amina.

Ndivyo itakavyokuwa kama unavyoamini.

320 Baba yetu wa Mbinguni, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, jalia maombi yangu, ninayoyaweka pamoja na ya ndugu yangu, matumaini yangu pamoja na matumaini yake, imani yangu pamoja na imani yake juu ya madhabahu Yako takatifu, yapokee, Bwana. Ninatoa haya kwa niaba yake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Ng'ang'ania sasa, lishikilie moja kwa moja. Mungu akubariki, ndugu yangu.

321 Baba yetu wa Mbinguni, walisema maombi ya imani humwoko mgonjwa yule, natoa yangu pamoja na ya ndugu yangu; ninamhurumia. Ee Bwana, ninaomba ya kwamba utamponya. Tusikie, Bwana, ninapoomba, katika Jina la Yesu. Amina.

Ubarikiwe, Ndugu, ng'ang'ania sasa, mwamini Yeye.

Njoo, dada yangu.

322 Baba yetu wa Mbinguni, ninaposimama hapa katika Uwepo Wako, na mbele ya kusanyiko hili, mbele ya mwanamke huyu, ninaomba, ninapoweka maombi pamoja na yake madhabahuni, utupokee, Baba. Ninatoa hili, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu awabariki. Ng'ang'anieni sasa, msi—msiikatishe.

Njoo, Dada. Je, ungetaka kwenda nyumbani, kula chakula chako cha jioni, upate afya? Endelea tu.

Unaamini, Dada?

Baba wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamponya, ninapotoa maombi yangu pamoja na yake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Ubarikiwe, Ndugu.

³²³ Baba yetu wa Mbinguni, ninaweka mikono yangu juu ya Ndugu, katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe. Ninatoa maombi yangu pamoja na yake, Baba, juu ya madhabahu Yako takatifu. Katika Jina la Yesu, jalia aponywe. Amina.

Mungu akubariki, Ndugu.

³²⁴ Sasa, kwa wasikilizaji, Yesu alisema maneno haya, Marko 11:24: “Amin, amin, nawaambia, ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka, wala usione shaka moyoni mwako, bali uamini kwamba yale uliyosema yatatimia, yatakuwa yako.” Mnaamini hilo? Vema, basi wekeaneni mikono, inamisheni vichwa vyenu. Wekeaneni mikono, msione shaka. “Sasa, ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka . . .”

Naam, mama? [Dada mmoja anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Loo, tutamwombea.

Bwana Yesu . . .

Sasa, wakati mkiomba, ninaomba, kwa ajili ya maskini . . . mama fulani aliyemleta mvulana mdogo hapa.

³²⁵ Baba, Mungu, ninaomba ya kwamba utatujalia uponyaji wa mvulana huyu mdogo. Sasa, ninaweka mikono juu yake, na kuamini katika Jina la Yesu ya kwamba itatendeka, ninapoweka imani yangu na mpendwa wake hapa, juu ya madhabahu yako, naomba apone, Bwana. Katika Jina la Yesu. Amina.

Amini, Dada. Ng’ang’ania, unaona.

³²⁶ Sijui tu, kuwaombea wagonjwa limekuwa jambo ambalo sijaweza kuelewa kamwe. Kabla sijatoka na upambanuzi ama chochote kile, kwa namna fulani, ningenda tu kuwaombea wagonjwa nilipokuwa, mhudumu wa Kibaptisti wa mtaani tu huko chini, kwa *namna moja ama nyingine* walipona tu, sijui.

³²⁷ Wengi wenu mmesoma hadithi kuhusu, hata Mungu kuwatuma wanyama huko, jinsi watu wamekuja kupitia ndoto na mafunuo, watu ambao hawajawahi kusikia hapo kabla wamekuja kutoka maili nyingi, na kuvuka bahari, wapate kuombewa. Ninaomba tu maombi ya imani, yote nijuayo, na ninaamini, ninaamini. Mungu aliliahidi, ndipo basi kama Yeye aliahidi kwamba . . .

³²⁸ Sasa haikubidi kuamini neno langu, liamini Neno Lake. Halafu basi . . . Ingekubidi kuamini neno langu kuhusu Yeye kuniita kuwaombea wagonjwa, lakini nafikiri ya kwamba Yeye amethibitisha hilo.

³²⁹ Angalieni hapa, miaka mingi iliyopita hapo nilipowaambia kuhusu Nuru hii kuu, Nguzo ya Moto, nikawaambia jinsi

ilivyoonekana, kabla haijapigwa picha yoyote ya kisayansi, sasa angalieni picha Zake walizo nazo.

³³⁰ Sasa, Nuru iyo hiyo imesimama papa hapa mahali nilipo sasa hivi, ninaiangalia moja kwa moja, papa hapa, Nuru yenye rangi ya zumaridi. Sasa, jicho hilo la kimitambo la kamera hiyo halipigi picha saikolojia, mwajua, hiyo Nuru ilikuwako. Hii hapa, ikifanya vile vile hasa lilisema ingefanya.

³³¹ Yesu alisema, “Nimetoka kwa Mungu, na ninaenda kwa Mungu. Bado kitambo kidogo ulimwengu hautaniona tena; hata hivyo ninyi mtaniona Mimi.” Sasa, hapa, Yeye alikuwa nini? Ile Nguzo ya Moto iliyowaongoza wale wana nyikani, ilifanyika mwili katika umbo la Mwanadamu, Yesu Kristo, Alikufa, akazikwa, akafufuka akaingia Mbinguni, na alipokuwa akienda zake Dameski Paulo alikutana na Nguzo ile ile ya Moto.

Unasema, “Loo, hilo ni kosa.”

Loo, la, yeye alisema, “Bwana, u Nani Wewe?”

Akasema, “Mimi ni Yesu.” Sasa, sasa, hakuna mmoja wa hao wengine aliyeliona, Paulo aliiona.

³³² Hakuna mtu mwingine aliyemwona huyo Hua, ila Yesu. . . juu ya Yesu ila Yohana, kwa sababu alijua atamwona, maana Mungu alimwambia hivyo. Mnaona? Jambo ndilo hilo. Aling'ang'ania, alijua jambo hilo. Sasa, Hii hapa.

³³³ Sasa, nilimwombea kila mmoja wenu, nilimwombea kila mmoja. Yesu alisema, “Ukiuambia mlima huu, 'Ng'oka,' wala usione shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba yale uliyosema yatatimia, yatakuwa yako.” Sasa, nimelisema, sasa na litendeke. Limeandikwa lipate kutamkwa; nimelinena, na litendeke.

³³⁴ Sasa hebu na tuombe, huku tumewekeana mikono, kama watoto wa Mungu wanaoamini. Kama uliwahi kushikilia, unawezaje kujiepusha na kushikilia sasa?


³³⁵ Kama ishara hizi kuu zingefanyika Urusi, isingekuwa ya kikomunisti leo hii. Ishara hizi kuu zingalifanywa huko—huko Uchina, isingekuwa ya kikomunisti leo hii.

³³⁶ Loo, Marekani, Marekani, ni mara ngapi Mungu amekuzuru, ni muda gani zaidi Yeye ataliruhusu? Wakati wa mwisho umewadia, nuru za jioni zinawaka.

³³⁷ Sasa, Bwana, ninawapenda watu hawa, ni watu Wako, na pamoja sisi ni ndugu na dada katika Mwanao, Yesu. Na sasa, Bwana, kama nilivyozungumza, usiku wa leo, juu ya Daudi na kombeo dogo, alivutiwa na kondoo wa baba, na haidhuru lilikuwa dogo jinsi gani, alikuwa tayari kuonyesha na kushinda kwa kile kidogo alichokuwa nacho cha kushindia, Nawe ulikuwa pamoja naye.

³³⁸ Bwana, ninawafuatilia kondoo hawa usiku wa leo, wamekuwa wagonjwa, nimetii amri Zako, ulionyesha Uwepo Wako, utayari Wako, umewaponya walio na kadi, wasio na kadi, ikionyesha ya kwamba Wewe upo hapa. Hushindwi kamwe, Wewe ni Mungu aliye kila mahali, nami ninakuja kumpa changamoto ibilisi ambaye angewaweka nyuma ya kizuizi cha sauti cha kutokuamini.

³³⁹ Mungu, ninawapitisha usiku wa leo, ninapasua njia kwa Neno la Mungu na—na kuwaweka huru. Katika Jina la Yesu Kristo, ninawarudisha kwenye malisho ya kijani kibichi yenye kivuli.

Toka, Shetani! 

62-0608 Kung'ang'ania
Aberdeen High School
Aberdeen, North Carolina Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org